# *Mara Nyingine Moja Tu, Bwana*

Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo tukifurahia karamu hii nzuri sana ya muziki, kuzifurahia nyimbo hizi wakati zinapoimbwa kwa shauku halisi. Nilikuwa nikimwangalia Jimmy, nafikiri ndiye, na kama tungeshikwa tu na shauku hivyo kuhusu mambo yote ya Mungu katika maisha yetu wenyewe kama Jimmy alivyo katika mhemuko wa wao kuimba, tungefika mahali fulani. Hakika ninamthamini mvulana huyo, baba yake, rafiki yetu mwema.

2 Ninataka kuwaulizeni swali. Hawa wasichana waliouimba huu, “Ningetaka Kulizungumzia Hilo,” hivi hilo ni kundi lile lile lililoimba miaka mingi iliyopita wakati nilipokuwa hapa? Hilo ni kundi lile lile? Nimejaribu kila mahali kuupata wimbo huo. Katika saa zangu zenye giza za majaribu, nimejaribu kuuwazia huo, “Ningetaka kulizungumzia hilo.” Jimmy Maguire, uliunasa huo kwenye kanda? Natumaini. Mnaona? Mmeuweka kwenye santuri? Na endapo iko, ninaitaka. Nami nimejaribu kuwazia hilo, nafikiri ya kwamba, “Yeye atanipenda wakati njia yangu ilikuwa imeingia giza sana.” Mnaona? Na hakika—hakika nimeufurahia wimbo huo mzuri wa Zayuni.

3 Sasa, nasikia, sina hakika na hili, lakini ninaamini kwamba kundi lili hili litakuwa likiimba kwenye Mkutano wa Wafanyabiashara, ninaamini, Jumapili, Jumapili ijayo. Nafikiri hiyo ni kweli, kama sikulielewa vibaya, saa nane Jumapili ijayo. Kwa hiyo kama unapenda uimbaji wa namna hii, mbona, watakuwa huko kutuimbia tena. Inatupasa kuwabeba kushuka Tucson kesho usiku, tuwaache waimbe huko chini. Ni—nina hakika ingekuwa ni baraka kwa watu.

4 Sasa, kesho usiku ni tawi la Tucson. Tutakuwa katika Hoteli ya Ramada kesho usiku, huko chini Tucson, ambapo nyote mnafahamu ya kwamba Phoenix ni viunga tu vya Tucson. Mnaona? Bila shaka tuna furaha kuwa nanyi nyote kama raia wenzetu wa uchumi wetu mkuu wa Arizona. Sasa, tuko juu ya kilima; ninyi mko bondeni; kwa hiyo, kumbukeni, yapata futi elfu mbili juu kuliko mlivyo ninyi, mnaona. Kwa hiyo viunga hivi vya mji, hakika tuna furaha kuwa hapa tukifanya ushirika pamoja nanyi usiku wa leo. Kwa hiyo kumbukeni kesho usiku na sehemu muhimu ya Arizona itakuwa ni dhi—dhifa ya tawi hili. Halafu basi kesho yake usiku tuko hapa kwenye, ninasahau jina la kanisa hilo sasa, ni Southside Assembly. Halafu Jumatano usiku tuko kwenye ya Kumi na moja na Garfield, naamini ndiyo,

Assemblies of God kule, kwa ajili yake. Ndipo basi Alhamisi mkutano unaanza.

5 Sasa, ninyi ni wazuri sana na tumekuwa na wakati mzuri sana juma hili, wa ushirika, na makanisa haya yote kote juu chini ya hili Bonde la Maricopa hapa. Naye Bwana hakika ametubariki kwa njia kuu, mno, kuliko nilivyomtarajia Yeye kufanya. Mahali pamekuwa pamejaa watu hata wakasongamana kwenye nyuga, huku watu wamesimama, na ushirika mkuu kwenye Neno. Wahudumu wametembea. Nimemwona mchungaji, Ndugu Outlaw, nimemwona katika kila ibada ambayo tumekuwa nayo, niwezavyo kukumbuka. Na wengine wamekuja tu kutoka kanisa moja kwenda lingine. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya, napenda hilo, kufanya ushirika mmoja na mwingine.

6 Kama vile mzee Ndugu Bosworth, ambaye amekuwa Utukufuni sasa miaka mitatu ama minne, yeye aliniambia, "Hivi u—unajua ushirika ni nini, Ndugu Branham?"

Nikasema, "Nafikiri ninajua."

7 Akasema, "Ni jamaa wawili wanaoshiriki meli moja." Kwa hiyo hiyo—hiyo ni kweli, jamaa wawili katika meli moja.

8 Kwa hiyo tunaangalia (nina furaha.) kwenye kusanyiko usiku wa leo, nikiwaona marafiki hapa ambao sijawaona hapo kabla, ambao wametoka huko mbali Kentucky na Indiana, kote huko juu Ohio, wameketi hapa, kututembelea. Hakika tuna furaha kuwa nao humu usiku wa leo. Labda wamekuwa katika mkutano huo mwingine, ila majengo makubwa, na kamwe sijawaona. Kwa hiyo Bwana awabariki sana.

9 Na sasa nitakaa tu kidogo. Sina budi kuendesha motokaa kuirudisha familia usiku wa leo, na inatubidi kuwa tayari kwa ajili ya ule mkutano kesho huko Tucson, kwa hiyo tunaenda huko chini usiku wa leo baada ya ibada. Hizo ni kama maili mia moja na ishirini na tano tu, na eneo kubwa la jangwa, nami nimeshikwa na usingizi na ni mchovu, kwa hiyo nitajaribu kuwaachilia muondoke.

10 Sasa, nilisema asubuhi ya leo, ya kwamba kama vile nilivyomleta nabii huyo juu ya kilima, mimi. . .Hiyo ilikuwa ni jana usiku, sivyo? Basi asubuhi ya leo tulikuwa tukizungumzia jambo lingine. Lakini sijali mkichelewa kwa ajili ya ninii. . .kwa ajili ya kazi yenu, wala sijali mkikosa siku moja mara kwa mara, ila msiikose shule ya Jumapili, mnaona, kwa hiyo tunawatakeni kwenye shule ya Jumapili.

11 Sasa, usiku wa leo, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi wake kwa maombi. Ninataka kusema kabla tu ya jambo hilo, kwa maskini kwaya hii ya kupendeza, hawa watoto wa Mungu, hakika ninawathamini, uimbaji wao mzuri. Naye Ndugu Moore aliniponyoka, nilikuwa nataka kumpa ibada hii. Lakini a—aliponyoka akaenda, ninamwona tu

mke wake mpendwa ameketi hapa. Kwa hiyo hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

12 Bwana Yesu, tunakuja tena usiku wa leo, kwanza, kukushukuru Wewe kwa yale yote uliyotupa. Na, zaidi ya yote ambayo umetupa, Uzima huo wa Milele unatokeza, kwa kuwa tunajua ya kwamba tutakutana tena; si tena katika dunia hii, katika dunia ijayo. Sasa libariki Neno Lako usiku wa leo. Nasi tunakushukuru Wewe kwa jinsi ulivyobariki uimbaji. Sasa ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaendelea kuubariki uimbaji, hizo nyimbo na waimbaji, mchungaji wa kanisa hili, wachungaji wenza, na pia mashemasi, wadhamini, na yote linayotetea. Wabariki, Baba.

13 Tunaomba ya kwamba utaubariki Ujumbe usiku wa leo, Maneno haya machache ambayo yamechaguliwa. Tunaomba ya kwamba Wewe utaliongezea muktadha, na kutupa baraka Zako. Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Jalia wanaume na wanawake usiku wa leo washike ono, wafahamu kilicho mpango wa Mungu kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Hilo tu ndilo tunalohitaji kufanya, ni kuingia tu katika mpango Wake, ndipo basi mambo hayo mengine yatajishughulikia yenyewe. Yeye alitufundisha hivyo, nasi. . . Yeye alisema, "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake, mambo mengine yote yataongezewa." Kwa hiyo jalia turudi usiku wa leo, Bwana, kwenye baraka za Ufalme, kwenye mpango wa Ufalme, na tujifunze Kwako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

14 Sasa, kidogo nimepwelewa tu na sauti kutokana na kuhubiri sana. Nami ninajua kuna joto humu ndani na ninawahurumia wote wanaosimama, hasa hao kina mama wanaosimama kuzizunguka kuta, huko kwenye ukumbi wa nje, nami nitaharakisha upesi tu iwezekanavyo, upesi tu niwezavyo. Basi wakati nikisoma ama kuhubiri, kumbukeni tu, Mungu aliye kila mahali sikuzote yupo hapa. Na kama vile ndugu mmoja alivyosema kuhusu yule mwenye kifafa wa wakati wa mwisho tulipokuwa hapa, Mungu anaweza kuponya kansa, ulemavu, chochote kile. Tayari amewaponya. Kama anaweza tu kuwafanya kuamini hilo! Huokolewi usiku wa leo, umekuwa mwokovu, uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Na sasa labda usiku wa leo utaukubali wokovu huo, lakini tayari umelipiwa, deni imelipiwa. Naye ibilisi aliyekuweka kwenye duka la rehani, Yesu alikuja akakukomboa na kuifungua milango, na jambo pekee unalopaswa kufanya ni kujitokeza na kudai uhuru wako. Hivyo tu. Unayo risiti kutoka kwa Mungu ya kwamba deni limelipwa. Yesu alisema, katika Maneno Yake ya mwisho, "Imekwisha!" Kila baraka ya ukombozi ilimalizika kabisa. Hasira kuu ya Mungu juu ya dhambi, hapo Yeye alipofanyika dhambi kwa ajili yetu, ilimalizika, deni lilimalizika.

15 Shetani hana nguvu tena, ila tu anavyoweza kudanganya nazo. Kama anaweza kukudanganya kuingia kwake, vema, itakubidi kuwa nalo. Lakini, kisheria, yeye hana nguvu hata kidogo, kila nguvu alizokuwa nazo alinyang'anywa pale Kalvari. Hapo ndipo gharama ilipolipiwa. Yeye si kitu ila mdanganyifu! Ukitaka kusikiliza udanganyifu wake, vema, sawa. Lakini, si lazima, uko huru usiku wa leo. Yeye amekufanya huru.

16 Na sasa kama kitu fulani katika Neno kinaweza kukufanya utambue ya kwamba wewe ni huru kwa neema Yake, ama kama kitu fulani, kutambua, nalo Neno linakufanya ufahamu, ama tendo fulani la Mungu, ya kwamba umehusishwa, inatuhusisha sote, basi likubali tu kwenye misingi hiyo, nawe uko huru, pia. Haikubidi kujisikia tofauti hata kidogo, haikubidi kujisikia chochote hata kidogo. Halijawekwa msingi juu ya...Yesu kamwe hakusema, "Ulilihisi"? Alisema, "Ululiamini?" Ni imani! Hiyo ni ninii yetu—hiyo ni ninii yetu—yetu...Imani ni—ni mkono, mkono wenye nguvu unaoshika Upanga mkali wa Mungu ukatao kuwili. Na huo Upanga mkali ukatao kuwili utakata na kuweka huru kila ahadi, kama mkono huo wa imani unaweza kuushikilia Upanga huo. Watu wengine wana shida ya misuli dhaifu sana nao labda wanaweza tu kukata mkwaruzo mdogo, wa kutosha kujiunga na kanisa. Wengine wanaweza kuingia katika kuhesabiwa haki. Wengine wanaweza kwenda kote hata kufikia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mkono mkubwa mno wenye nguvu, ukiishika Biblia hii, unaweza kukata na kuweka huru kila ahadi. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo iweni na nguvu katika Bwana!

17 Sasa nataka kusoma usiku wa leo kutoka kwenye muktadha mdogo ambao ni—nimeandika muhtasari kidogo hapa chini. Unapatikana katika Kitabu cha Waamuzi, mlango wa 16 wa Waamuzi, vifungu vya 27 na 28, kuchukua muktadha wa yale ninayotaka kusema.

> *Basi nyumba hiyo ilikuwa imejaa* mume *kwa wake;... wakuu wote wa Wafilisti walikuwamo humo; na juu ya dari palikuwa na watu elfu tatu* waume *kwa wake waliokuwa wakitazama, wakati Samsoni alipocheza.*
>
> *Samsoni akamwita BWANA, akasema, Ee BWANA MUNGU, unikumbuke, nakuomba wewe,...ukanitie nguvu, ninakuomba, mara hii tu, Ee* Bwana *Mungu, ili nipate...kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.*

18 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno. Kama yanipasa kuliita somo, ningetaka kuchukua hili kwa dakika chache zijazo, "Bwana, mara hii moja tu tena," *Mara Nyingine Moja Tu, Bwana.*

19 Kulikuwako na yapata, kama Maandiko yasemavyo, yapata Wafilisti elfu tatu wakiangalia chini kutoka kwenye sakafu ya

juu ya huo uwanja wa michezo, wakati hawa wawili walipoingia kwenye uwanja huo mkuu, ama uwanja mduara; majemadari wa vita walioheshimika sana, wanawake wao waliopambwa vito vizuri sana, wakati wakiketi mahali hapa. Ndipo mtangazaji akasema, kwamba, “Samsoni aingia kwenye sakafu ya chini.”

20 Hapana shaka walisimama, wakasogea karibu kidogo, wakanyosha, tuseme, shingo zao, wapate kuona vizuri. Nao wangeweza kuona nini ila bonge la mwili wa mwanadamu, mtu ambaye wakati mmoja alikuwa ni shujaa mkuu, akiongozwa, kipofu, jinsi alivyokuwa, akiongozwa na mvulana mdogo aliyemwongoza hata kwenye sakafu ya chini. Siku nzima, kumbi zilirudisha mwangwi ukuta kwa ukuta kwa shamrashamra za wanawake na wanaume walevi. Hiyo ilikuwa ni tamasha ya jinsi gani! Ni unyamavu wa jinsi gani hapana shaka ulikuja juu ya hilo jengo, wakati mtu huyu, akiongozwa na mvulana mdogo, adui wao mkubwa sana, alipojitokeza akitembea sakafuni, bila macho, ilibidi aongozwe na mvulana mdogo. Mtu ambaye alikuwa ni mtu hodari sana! Mtu ambaye alikuwa shujaa kama Samsoni alivyokuwa, na halafu alazimike kuongozwa na mvulana mdogo, hapo sakafuni. Na mtu ambaye alikuwa ni mtumishi wa Mungu, aliyeletwa katika hali hii, katika mahali hapa pa shamrashamra za ulevi.

21 Ilikuwa ni sherehe kubwa kwa mungu wao, Dagoni, mungu samaki aliyekuwa amepata ushindi dhidi ya Yehova. Hebu tusimame kwa dakika moja tuache hilo lipenye, kusherehekea ushindi dhidi ya jeshi la Yehova. Dagoni, ile sanamu ya kikafiri, mungu samaki wa Wafilisti, ambaye Mungu alimchukia. Nao hawa hapa katika ghasia za ulevi wao, wakisherehekea ushindi dhidi ya mtumishi wa Mungu kushindwa. Hilo ni jambo baya sana jinsi gani kuwazia! Ningetaka, kama ingaliwezekana, kusimama kimya dakika chache na kuchora picha ya hiyo. Lakini liwazie tu niani mwako, kama ingekubidi kusimama na kuangalia jambo kama hilo. Ndipo nitairejesha picha hiyo moja kwa moja kwako.

22 Wazieni tu, siku nzima, wakinywa, kusherehekea, wanawake waliovalia nadhifu, wanaume, majemadari wa vita, mashujaa, watu mashuhuri wa taifa wamekusanyika katika jengo hili jipya ambamo walikuwa wameweka sanamu mpya ya mungu samaki, wakimtolea heshima na sifa kwa ajili ya ushindi dhidi ya watumishi wa Yehova. Sasa, kuifanya mbaya zaidi, huyu hapa kiongozi anakuja, mjumbe wa siku hiyo, huku macho yake yameng’olewa, akiongozwa na mkono wa mvulana mdogo, kumwingiza kwenye uwanja wa michezo. Mtoto huyo alimwongoza huyo kipofu aliyekuwa akijikwaa katika mahali hapo, nami ninaweza kusikia mnong’ono kutoka kwa m—mtu huyo mkubwa mno amesimama pale kama mtambo mkubwa mno, bali asiyejiweza kabisa. Mungu alikuwa amemwinua kwa ajili ya kusudi fulani. Akauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza;

naye huyu hapa amesimama, mtambo mkubwa mno usio na nguvu ndani yake, ukiongozwa na mvulana mdogo. Lakini hapana shaka, niani mwangu, ya kwamba Samsoni alikuwa amewazia mambo haya yote. Wakati alipokuwa amepoteza nguvu zake, alikuwa amewazia yaliyokuwa yametukia. Nadhiri yake ilikuwa imeondolewa kwake naye alikuwa amejisalimisha kwa adui wake. Nao, kwa kujilipizia, walikuwa wameyang'oa macho yake. Ndipo akamwambia maskini mvulana yule, "Niongoze kwenye nguzo ambapo kuna mhimili ambao jengo hili linaukalia, niongoze tu kwenye nguzo hii."

23 Basi liwazieni! Walikuwa wamemweka huko nje, wakimdhihaki, akiliburudisha kundi hilo la walevi. Ilikuwa ni aibu jinsi gani! Hiyo ilikuwa ni fedheha jinsi gani! Huo ni mfano wa jinsi gani! Kuninii. . .Inanikumbusha juu ya taifa lililoshindwa ambalo limeoza kimaadili, wakati Samsoni aliposimama karibu na mhimili huu, akimburudisha adui. Ameaibishwa na kuvurugika, ni hali ya jinsi gani aliyokuwa ndani yake! Ni mfano mzuri sana wa taifa lililoanguka, taifa potovu kimaadili, kanisa lililoanguka ambalo liliuza haki zake za mzaliwa wa kwanza, likaoza kimaadili, na kujisalimisha kwa adui. Mfano wa umma, ingawa uliinuliwa kumtumikia Mungu, lakini kuoza kimaadili kunakuingiza katika hali hiyo. Huo ulikuwa ni mfano wa jinsi gani!

24 Ninaweza tu kuwasikia mashujaa wote huko, wanawake wote pamoja na shanga zao na mikufu na vito vizuri, na kadhalika, wakisema, "Kumbe huyu ndiye Samsoni? Huyu ndiye mtu yule mwenye nguvu ambaye mmesema habari zake. Huyu ndiye mtu yule mliyesema roho ya miungu mikuu iliishi ndani yake. Huyu ndiye mtu ambaye angeliliteka taifa letu, mliyesema habari zake, lakini hebu mwangalieni sasa!"

25 Ni mfano wa jinsi gani! Ni somo la jinsi gani hilo linalopaswa kuwa kwetu! Ni jambo lenye uchaji jinsi gani linalopaswa kuwa. Hatupaswi kulikaribia hili kana kwamba tu ni kukusanyika pamoja na kuwa na wakati mzuri katika sherehe. Tunakusanyika pamoja kuona mahali tunaposimama, kuona ni jambo gani linaloendelea kwetu sisi.

26 Nami ningeweza kusikia, na Samsoni, hapana shaka, angeweza kusikia kutoka upande mmoja, huo mwingine, wa watu ambao walikuwa wamesikia habari zake. "Vema, na kwa hiyo ati huyu ndiye Samsoni!"

27 Ninashangaa, leo hii, kama adui hawezi pia, kwenye wakati huu, kusema jambo lile lile kuhusu huduma yetu ya Kipentekoste.

28 Kutaja tu jina Samsoni, wote wangeingiwa na wasiwasi, kwa sababu alikuwa mtumishi wa Mungu aliyetiwa mafuta. Alizaliwa na karama ya Kinadhiri, nao walijua kwamba hapakuwapo na chochote kingaliweza kuikomesha karama

hiyo ya Kinadhiri mradi tu aliishikilia. Yeye alikuwa ni mtu wa Mungu aliyechaguliwa wa siku hiyo, mjumbe wa Mungu aliyechaguliwa wa siku hiyo. Wengi wao waliwazia kile hii haina budi kuwa. Wengi wao walimkumbuka. Wengi walikumbuka, wakati wakikiangalia kiumbe hiki kisichojiweza kimesimama pale huku kimeikumbatia hiyo nguzo, kipofu. Wakimdhihaki, wakimpiga kwa mijeledi, wakisema, "Hima, Samsoni, ewe mtu mashuhuri mwenye nguvu! Fanya jambo kulihusu! Wewe uliye na nguvu sana, yuko wapi Mungu wako?"

29 Kama hivyo sivyo tu karibu vile adui anavyopenda kufanya wakati anapoweza kukuweka chini! Lakini hawezi kuthubutu kujaribu hilo mradi tu nguvu za Mungu zinafanya kazi kupitia kwa Kanisa. Yeye ni—angeogopa kufanya hivyo wakati baraka za Kinadhiri zikiwa juu yako. Lakini kama anaweza kukuona umeshindwa, hapo ndipo anapokudhihaki. Hapo ndipo anapoweza kusema hakuna tofauti kati yao na sisi, hao ni wanadamu tu kama tulivyo sisi. Lakini wakati kuna kitu tofauti, kitu cha kipekee kikiwa na baraka za Yehova juu yake, basi wanaogopa kusema lolote. Mradi tu wanaweza kuona nguvu hizo za Mungu zikitenda kazi, ibilisi ana akili za kutosha kufunga kinywa chake. Lakini wakati anajua umeshindwa, yeye anamfungulia kila ibilisi awezaye (kumwachilia) juu yako.

30 Hiyo ndiyo hali aliyokuwa amesimama Samsoni. Hebu tuwazie tu, kwa kuwa naweza kuwaona hao mashujaa, baadhi yao ni askari wakongwe wastaafu wenye makovu nyusoni mwao, wakati wakimwangalia Samsoni amesimama pale, bila matumaini na hajiwezi, walikumbuka wakimwona amesimama wakati mmoja na mfupa wa taya mkononi mwake, na Wafilisti elfu moja wamelala maiti miguuni pake. Na sasa mvulana mdogo anamwongoza kote kwa mkono. Wangekumbuka jinsi walivyouliza maswali katika halmashauri yao, hapo habari ilipoletwa ya kwamba mtu, mtu tu, alichukua ninii . . . mfupa wa taya ya kale ya nyumbu, uliochomwa na jua, ulioungua.

31 Na, sasa, wengi wenu wamesoma historia ya Wafilisti. Silaha hizo walizovaa watu hao, zile kofia za chuma vichwani mwao zilikuwa na unene wa karibu inchi moja ya shaba. Na koti lao walilovaa, walikuwa ni watu wakubwa wenye nguvu, pamoja na vipande vikubwa vya nusu inchi ya shaba juu chini mwilini mwao, kuukinga na mkuki mrefu unaokuja, ama pi—pigo la nguvu kwa upanga ukatao kuwili ambalo lingewaangusha chini.

32 Sasa, mtu angewezaje, mtu mmoja tu, amezungukwa na elfu moja, wenye silaha, nao ni mashujaa waliovaa silaha na wana mikuki, hizo chepeo kubwa ambazo jicho tu ndilo lililoonekana, mtu angewezaje kuchukua mfupa wa taya la nyumbu na kuwapiga elfu moja wa hao wakati mmoja? Mbona, pigo la kwanza kwa huo mfupa wa taya mwepesi wa kuvunjika, ungesambaratika vipande-vipande juu ya moja ya hizo chepeo. Walijua ya kwamba Nguvu fulani za Kimbinguni, wakati

alipompiga shujaa huyo kichwani, kitu hicho kilibonyea ndani na kumwua mara moja. Mkono wa kuume na mkono wa kushoto, alipiga, na kila alipopiga, nguvu za Mungu zilipiga pamoja nao.

33 Haihitaji, kile tungewazia, kitu kikubwa, inahitaji tu m—mkono uliotiwa mafuta kabisa na Roho Mtakatifu, pamoja na nguvu za Mungu, kumwangusha adui yeyote chini ya hali yoyote ya mambo.

34 Na jinsi mashujaa hao walivyokumbuka! "Ingewezekana kwamba tulishika mtu mwingine?" baadhi yao huenda walisema. "La, huyo ni yeye. Ninaweza tu kuona umbo lake, huyo ni Samsoni, yule aliyetumikia kile alichosema kilikuwa ndicho Mungu wa kweli. Lakini Mungu wake hakika amemwacha."

35 Lakini walikosea! Mungu hakuwa amemwacha, yeye alikuwa amemwacha Mungu. Nami nafikiri hivyo ni kama ilivyo na watu usiku wa leo. Sio Mungu ameliacha kanisa Lake, ni kanisa limemwacha Mungu pamoja na Neno Lake. Na hiyo ndiyo shida.

36 Angalia, wengi wao walikumbuka. Lile kundi lililosimama upande mmoja, lilisema, "Ninaweza kukumbuka wakati Delila alipomchukua na kumfunga kwa kamba ambazo hata farasi wasingeweza kuzitenganisha. Na wakati tulipomvamia, jinsi ambavyo zilikuwa kama nyuzi ndogo, alizivunja tu vipandevipande. Naye huyu hapa amesimama, ameshindwa."

37 Pia kundi lingine lingekumbuka usiku mmoja huko chini Gaza, jinsi ambavyo walimzingira ndani, bali angali alikuwa na upako juu yake. Basi wakajaribu kumzingira ndani, na kumfungia malango. Wakasema, "Sasa, tutamvamia ghafla." Lakini Roho wa Bwana akamrudia, naye akayanyanyua malango hayo yote na kupanda nayo juu ya kilima.

38 Mtu anapokuwa kwenye wajibu wake kwa ajili ya Mungu, hakuna lango, hakuna chochote kinachoweza kumzuia. Ibilisi alijaribu kumzingira mtu wa Mungu na watu siku moja, kwa Bahari ya Shamu, bali akapitia moja kwa moja kati yake haidhuru. Wakati mradi tu mtu yuko katika utumishi wa Mungu, mradi tu upako na baraka ziko juu yake, hapaswi kuogopa chochote, kwa sababu Yeye ametuahidi atakuwa pamoja nasi, wala hakuna kitu kitakachotusumbua kwa vyovyote vile.

39 Lakini huu ni mfano wa kile kinachotukia wakati Mungu, uvumilivu Wake, hatimaye unakwisha juu yako. Sasa, Yeye ni mvumilivu, lakini, kumbukeni, subira Yake ina kikomo. Sasa, Samsoni alikuwa akifanya makosa usiku ule ule walipomzingira kule chini, bali hatimaye Mungu akatosheka nalo! Asingeweza kumsahihisha. Ombi langu ni, kwamba, "Mungu, kamwe asiliache kanisa hili la Kipentekoste lifikie mahali ambapo subira ya Mungu imekwisha kwenu." Yeye atawatuma wajumbe, kama tulivyofundisha juma hili, akiwainua manabii kote katika

nyakati, wakilitabiri Neno Lake na kulirejesha Neno Lake, halafu mnaendelea kuliondokea. Mtajikuta mmepofushwa, pia, bila nguvu, wasiojiweza, walioshindwa, nami ninahofia huko ndiko tunakoelekea. Mnaona, Samsoni aliangukia madoido. Jambo lile lile ambalo kanisa siku hizi linaangukia, madoido. Ni sikitiko jinsi gani kuona mambo haya yakitukia.

40 Naam, wakati walipojaribu kuziwekea uzio nguvu za Mungu, walikuta kwamba wasingeweza. Samsoni aliyanyanyua malango hayo makubwa ya chuma, ambayo yangalikuwa na uzito wa tani kadhaa, akaenda kilimani nayo na kuyaweka chini. Bila shaka, hakuna mtu angalithubutu kumfuata, wanajua vema zaidi!

41 Basi mtu anapokuja katika upako wa Roho Mtakatifu, na pamoja na Neno la Bwana, akiwa na BWANA ASEMA HIVI, heri uwe na akili bora zaidi kuliko kujaribu kulishambulia Hilo, maana utakuta kuna mkono wa Mungu aliye hai, nao ni mzito.

42 Lakini tunaona ya kwamba kulikuwako na kundi lingine pale ambalo siku moja lilimwona njiani mwake akishuka, naye simba akamkimbilia, na kunguruma. Na simba ni mnyama hatari ambaye anaweza kumwua mtu punde tu, wanne ama watano wa hao, shambulizi moja tu ndilo analohitaji. Basi simba huyu, akiisha kusumbuliwa, nao waliona tukio hilo wakati wakimwangalia huyo simba. Naye huyo simba, labda alisumbuliwa, na alikuwa na hasira, ndipo akaruka mbio kumfuata Samsoni. Naye huyo hapo amesimama, hajiwezi. Lakini, mara ghafla!

43 Loo, Yeye ni Msaada uliopo karibu sana wakati wa shida! Mara ghafla! Kwa nini ninyi watu wagonjwa msiliwazie hilo usiku wa leo? Kwa nini ninyi mnaohofia kwamba mtu fulani atasema jambo fulani dhidi yenu, jambo fulani kuwahusu? Walilisema kumhusu Yesu. Mara ghafla, alitegemea nguvu za Mungu! Na kila mmoja wenu, kupitia maungamo na imani, anategemea nguvu zote zilizopo, Mbinguni na duniani pia, kuja juu yenu.

44 Samsoni, wakati akisimama pale, nguvu za Mungu zilikuja juu yake, naye yule simba alimrukia, alimshika tu kwa kinywa na kumrarua kwa mkono wake. Basi mtu huyo ambaye angefanya kitu kama hicho. . .Huyu hapa mtu yule yule amesimama, ameshindwa, hajiwezi, na ni kipofu.

45 Nami karibu ningeweza kuwaonyesha kanisa kama hilo, halijiwezi, limeshindwa, na ni kipofu, likizikataa ahadi, likilikataa Neno, kanisa ambalo Kristo aliahidi ya kwamba lingekuwa na nguvu juu ya maradhi. "Katika Jina Langu watatoa pepo," kumchukua ibilisi na kumtoa, na baraka alizoliahidi kanisa Lake. Basi kwa sababu kanisa limeondokea mikutano ya maombi, na kutoka kwenye uaminifu, na kuifanya dini ya Kristo mapokeo, na limeondoa nguvu zote kutoka kwake.

Madoido yameingia makanisani mwetu, nalo limesimama karibu limeshindwa. Loo, jamani!

46 Huyo hapo amesimama, amevuliwa nguvu zote, na mwanamke, kwa sababu tu macho yake yalianza kutamani, kwa sababu Yezebeli fulani mzinifu alianzisha mfumo wa kumshinda mtumishi wa Mungu.

47 Naomba niseme hili kwa uchaji, kumeundwa mfumo wa Yezebeli, ambao unashinda, ukiyaleta yote katika muungano, madhehebu yote, Wapentekoste na mengine yote, kuwaingiza kwenye Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo si zaidi ya mtego wa ibilisi, kuwanyang'anya mlicho nacho. Halafu atawacheka. Mmevuliwa nguvu, na mwanamke huyo!

48 Pentekoste, miaka michache iliyopita, si zaidi ya miaka hamsini iliyopita, ilitokeza wazi. Watu walikuwa ni tofauti. Walitoka kwenye—kwenye makundi mbalimbali ya kilimwengu, kwa sababu ya mambo yao ya kilimwengu, na kujitokeza kama mfano. Naye Mungu amelichukua kanisa hilo, na leo hii ni moja ya makanisa yenye nguvu sana ulimwenguni. Lakini jambo ambalo linafanya, limegeuka moja kwa moja nyuma na kurejea kwenye mkusanyiko ambao liliitwa litoke kwake. Basi linapoanza kufanya hivyo, nguvu zake zinaondolewa kwake. Tunapata wapi mkutano wa maombi ya usiku kucha? Acha mhubiri ahubiri mpaka yapata saa saba ama nane usiku kama alivyozoea kufanya, atakuwa akihubiria viti vitupu, hawana budi kwenda nyumbani wakaone *Tunampenda Susie* ama mtu fulani kwenye kipindi fulani cha matangazo ya televisheni. Sasa, hiyo ni kweli! Kwa nini? "Zilipo hazina zako, hapo ndipo moyo wako ulipo pia." Hazina zetu zinapaswa kuwa katika Neno! Watu wa Arizona ni watafuta madini, inawapasa kwenda mkachimbe kwa kitambo kidogo, mnaona, muone mna nini.

49 Lakini hapo alisimama Samsoni, ameshindwa, amevuliwa na mwanamke. Nguvu zake zote ziliondolewa kwake kwa sababu yeye alijisalimisha na kutoa siri yake kwa mwanamke.

50 Sasa, mara tulipokuwa wakubwa vya kutosha hata tungeweza kuondoka pembeni na kuondoka kwenye maskini misheni ndogo mahali fulani, tunajaribu kujenga makanisa yaliyo makubwa kuliko jamaa huyo mwingine. Tunataka kuwashinda Methodisti, Presbiteri, Baptisti. Hilo silo kusudi lenu! Hiyo siyo sababu ya ninyi kuwa jinsi mlivyo. Mungu tayari alikuwa na hilo. Yeye hakuwainua kwa ajili ya jambo hilo. Aliwainua kama mfano apate kuweka nguvu Zake ndani yenu, apate kuonyesha utukufu Wake.

51 Lakini hebu akina Ricky wachache waingie mle, nao watalipindua na kwenda kuyafuata mambo ya madoido ya duniani. Karibu makusanyiko yote yanataka mvulana mdogo awe mchungaji wao, aliye na nywele nzuri sana za kipilipili, nanyi mnafikiri ya kwamba anajua mengi juu Yake kuliko

mtu mwingine yeyote. Lakini hebu mwili wako ushikwe na ugonjwa wakati mmoja, na hutaki mmoja wa maskini madaktari hawa ambao ndio kwanza watoke shuleni, kama unaenda kufanyiwa upasuaji na moyo wako ufanyiwe upasuaji, unamtaka mzee mwenye mvi, ambaye amekuwa na uzoefu. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo ni Injili ya mtindo wa kale ambayo imethibitishwa kwamba ni nguvu za Mungu, sio baadhi ya hawa maskini akina Ricky ambao seminari zetu zinawaangua. Mnajua jambo hilo. Hapo ndipo tulipo usiku wa leo, hiyo ndiyo hali tuliyomo. Hamna shughuli kuingia kwenye machafuko kama hayo, kwa vyovyote vile. Mlianza kuanguka papo hapo, na kamwe hamjarudi, wala hamtarudi mradi tu mnazidi kwenda.

52 Hivi mliwahi kuwazia, wakati hao Wafilisti walipokuwa wakimshangaa Samsoni, hivi ulipata kuwazia ni kitu gani kilichokuwa kikipitia akilini mwa Samsoni? Unafikiri ni kitu gani kilichokuwa kikipitia akilini mwa mtu huyo? Ninaamini alikuwa akiwazia, wakati akiwa pale, hata hivyo kipofu kabisa, asiweze kuona tena, alikuwa akitafakari juu ya ushindi wote mkuu ambao Mungu alikuwa amempa. Huyo hapo, akitafakari juu ya siku zilizokuwapo, kile walichokuwa wakifanya.

53 Na hivyo ni karibu tu jinsi mwanadamu alivyo, kama nilivyosema hapa wakati fulani uliopita. Mwanadamu sikuzote anayatafakari yale Mungu aliyofanya, na kutazamia yale Mungu atakayofanya, bali akipuuza yale Mungu anayofanya. Mnaona? Angalia anayofanya sasa! Tunayajua yale amekwisha fanya. Naye anatutumia na kujaribu kutuchochea tena, akijaribu kuturudisha kwenye njia ya Neno Lake, na kulithibitisha kwa Neno Lake lililothibitishwa. Nasi tunaketi tu, tunalala, tunaenda nyumbani, tunasema, "Alisema nini? Nachukia kwenda kuwasikiliza wakipiga makelele kwa muda mrefu hivyo."

54 Hilo lilikuwa likiingia niani mwake, kile tungalikiita "siku yake ya mafanikio makuu," huko nyuma wakati alipokuwa katika Roho wa Bwana, wakati Bwana alipojibu maombi yake. Hata kabla hajaomba, mradi tu alimwishia Mungu, Mungu alikuwa hasa kwenye wakati unaofaa. Hakuwa na wakati wa kuwaza kuhusu, "Vema, sasa, sina budi kuomba vya kutosha sasa na kuona kama hawa Wafilisti elfu moja . . . " Yeye alijua Mungu alikuwa pamoja naye, hapakuwapo na hukumu, kwa hiyo alinyakua tu kitu cha kwanza alichoshika mkononi mwake, akaanza kuwapiga. Hiyo ni kweli. Hakungojea mpaka alipopata Shahada ya Sanaa, ama kujifunza jinsi ya kupigana kwa upanga, alichukua tu kile kilichokuwa mkononi mwake na kuanza kupiga vita nacho.

55 Lakini siku hizi tumejifunza namna ya kupigana na kanuni zote za imani, na kila kitu namna hiyo, na kuzozana na kushambuliana, hatufikii mahali popote. Sisi ni wadanganyifu, kama ilivyokuwa katika siku za Goliathi. Labda Mungu

atatupelekea Daudi fulani asiyezijua kanuni za imani, bali anajua tu nguvu za Mungu ambazo zimepimwa na kujaribiwa. Hapo kanisa zima lilikuwa limesimama, limeshindwa, kwa sababu jamaa fulani mkubwa alikuwa akisema kwa sauti kuu, "Siku za miujiza zimepita." Lakini haikufanya kazi wakati mtu wa Mungu alipokuja pale, maskini jamaa mdogo, mwenye mabega yaliyoinama, aliyeonekana mwekundu. Lakini Mungu alikuwa pamoja naye, alikuwa na ujuzi.

56 Nao wakasema, "Chukua hii hapa kanuni ya imani ya kanisa letu, uende kule ukakabiliane naye."

57 Akasema, "Kamwe sijakithibitisha kitu hicho, sijui chochote kukihusu." Akaja kujua, ya kwamba, fulana ya kikasisi ya Sauli haikumwenea mtu wa Mungu, kwa hiyo akakitupilia mbali kitu hicho na kuchukua kile alichojua ni cha kweli.

58 Na, leo hii, hatuhitaji Shahada ya Sanaa, wala—wala digrii fulani ya uzamifu, kuingia kwenye kanisa fulani au kitu fulani. Kitu pekee tunachohitaji ni nguvu na ufufuo wa Kristo maishani mwetu, kulichukua Neno la Mungu, pamoja na upendo wa Mungu mioyoni mwetu, ambapo tuna hakika ya kwamba Mungu atayajibu tuyaombayo.

"Hatawanyima kitu chochote chema hao waendao mbele Zake kwa ukamilifu."

59 Sasa, yeye alitafakari juu ya siku zake kuu, wakati kulipokuwapo na siku kuu. Kanisa usiku wa leo linawazia huko nyuma yapata miaka kumi na mitano iliyopita, kwenye uamsho wa uponyaji wa Kiungu, juu ya ushindi. Sasa, na yeye pia . . . wa Mungu, na watu Wake waliokuwa wameshindwa. Hilo linapaswa kuwa ni baya vya kutosha, kwamba Samsoni angesimama na kuwazia kwamba alikuwa amemkosea Mungu. Yeye, haikuwa ni kosa la Mungu kwamba yeye alishindwa, ilikuwa ni kosa lake mwenyewe. Na ya hao watu, watu wa Mungu, aliokuwa ameinuliwa kuwahubiria Injili, katika nguvu zake, na kwa kubembana na mwanamke huyu mtovu wa uadilifu, mwanamke mzinifu, alikuwa amepoteza nguvu zote ambazo Mungu alikuwa amempa.

60 Ndivyo imekuwa na kanisa! Mungu aliliinua kanisa lipate kuwa ni mnara wa taa, kuziachilia nguvu Zake, kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kuwatoa pepo, kuishi kitakatifu, kuihubiri Injili yote, kuidhihirisha, bali tunaanza kujipenyeza ndani na kushusha viwango.

61 Tulichukua mifano mibaya. Wanawake walimwiga mke wa mchungaji. Yeye alimwachilia aingie wazimu, kukata nywele zake, kuvaa namna yoyote ya nguo za kizinifu, kamwe hakumkemea. Nao hao wanawake wengine wanasema, "Kama Dada *Nanii* anaweza kufanya hivyo, mimi pia ningeweza." Usimfanye huyo mfano wako. Unaona? Mungu alikwambia jambo la kufanya, dumu na Hilo.

62 Sasa, basi unapofanya hivyo, unamkosea Mungu na pia unawakosea watu Wake, kuwakosea watu Wake. Unapowakosea, unamkosea Mungu. Mungu alikuweka hapo upate kuwa mlinzi, basi unapoiona dhambi ikinyemelea ndani, badala ya kukikatilia mbali kitu hicho, wanakichochea. "Wakati viongozi wote wa jimbo wanapokusanyika pamoja, tutakuwa na jambo fu—fulani, tutapigia kura fundisho fulani hili tuliondoe kanisani, la uponyaji wa Kiungu. Ha—hatulipendi." Ndipo mnaanza kupiga kura dhidi ya Hilo. Loo, ni, hivyo ndivyo ilivyotendeka.

63 Methodisti, ninyi Methodisti mlikuwa na uponyaji wa Kiungu makanisani. Presbiteri, Lutheri, mlikuwa nao muda mrefu uliopita, mlikuwa na kupiga makelele na furaha. Ni nini kiliifanyikia? Mlilipata kundi la wahuni elfu moja mia nane na kitu waliokichukua kitu hicho wakakipeleka kwa madoido, nacho kikaondoka.

64 Nanyi Wapentekoste mmefanya jambo lile lile! Hiyo ni kweli! Na sasa mnasimama mmeshindwa tu kama hao wengine, nyote mmejiundia madhehebu, "Nasi kundi hili, tunaamini *hivi*. Na kama wewe si mfuasi wetu, utaenda kuzimuni." Basi mnafanya nini, kubishana? Hamwendi popote. Mungu Mwenyewe hawaonyeshi upendeleo wowote, maana mmesimama mmeshindwa tu kama hao wengine, kwa maana mlipitia njia ile ile waliyopitia. Kweli kabisa!

65 Sasa yeye alikuwa ni mfungwa wa—wa taifa alililoinuliwa apate kuliangamiza. Huyu hapa alisimama yule mtu mwenye nguvu amesimama pale, mfungwa wa taifa lile lile alililoinuliwa na Mungu kuangamiza.

66 Sitaki kuwaudhi, bali natumaini litawasaidia. Nalo hili hapa kanisa la Kipentekoste linakuja ambalo Mungu aliliinua, akalivuta kutoka kwa dhehebu, ambamo liliwaingiza, na sasa ninyi ni mfungwa wa dhehebu lile lile. Sasa, mnajua hiyo ni kweli! Halafu hebu mtu fulani aseme jambo fulani dhidi yake, mko tayari kuwatupa nje. Ni karibu "kipofu akimwongoza kipofu."

67 Na mtu yeyote anajua ya kwamba kanisa la Kipentekoste, miaka hamsini iliyopita, lilikuwa likikemea kila kitu ambacho kingejiundia dhehebu. Mlikuwa ni ndugu na dada, nanyi mliishia wakati huo. Nanyi mlizungumza kuhusu kanisa la kisasa na mitindo yake, na wanawake jinsi walivyotenda, na mitindo waliyokuwa nayo, na wanaume, na kulikosea Neno la Mungu. Naye Mungu akawaita mtoke kwa hilo. Ndipo mkageuka moja kwa moja na kurudi moja kwa moja katika kitu kile kile ambacho Mungu aliwaita mtoke kwake. Na sababu yenyewe ya Mungu kuwainua kuwa hivyo, mmesimama huku mmefungiwa kwenye nguzo ya dhehebu fulani; mmeshindwa tu kama Samsoni alivyoshindwa, huku macho yenu yameng'olewa, msilione Neno,

na kila kitu kingine. Hiyo ni kweli. Ni vibaya sana. Mungu aliwainua kukishinda kitu hicho, nanyi mmejiunga nacho.

68 Ndipo Samsoni akageuka moja kwa moja na kumwoa mwanamke, akaoa moja kwa moja kwenye kitu kile ambacho Mungu alimtoa kwacho. Nalo kanisa, kanisa la Kipentekoste, liligeuka moja kwa moja na kuoa kwenye kitu kile kile ambacho Mungu aliwatolea. Hawezi kulishughulikia kundi, Mungu hushughulika na mtu binafsi. Daima imekuwa ndiyo sera Yake. Watu wawili wana mawazo mawili mbalimbali. Mungu hushika mtu mmoja ndani Yake, huyo tu ndiye inambidi kuwa naye, mtu mmoja! Hilo ndilo analojaribu kufanya leo hii, anajaribu kukushika mkononi Mwake, atamchukua mmoja hapa na mmoja pale. Kamwe haitakuwa ni kundi fulani, kwa hiyo liondoe tu hilo niani mwako.

69 Unapounda dhehebu, papo hapo unapoteza ninii yako... unapoteza haki yako ya mzaliwa wa kwanza. Ninataka kumwuliza mtu yeyote, ni wakati gani uliwahi kumwona m—m—mtu akiinuka akiwa na ujumbe wa Mungu, na mara alipoondoka duniani wao wakauundia dhehebu, mara walipounda dhehebu, lilikufa wala kamwe halikurudi tena. Hakuna fungu moja—moja la Maandiko popote, hakuna kipande hata kimoja cha historia, hakuna kifungu kimoja cha historia, ambacho—ambacho kinaonyesha ya kwamba dhehebu lolote, ama kundi lolote la watu lililowahi kuunda dhehebu, walipoteza nguvu zao za kiroho na kamwe hawakurudi tena, wala si nyumba ya Mungu aliye hai, kipimajoto cha kiroho ni arobaini chini ya sufuri wakati wote. Hivyo ndivyo ilivyo, "Mfano wa utauwa, wakikana Nguvu zake, hao nao ujiepushe nao."

70 Mungu, katika siku hizo, daima alimwinua mtu fulani ambaye angekilipua kitu hicho moja kwa moja kutoka kwenye msingi wake, na kulichukua kundi hilo dogo, kanisa lililosalia, na kulipeleka kwenye ushindi. Atafanya hivyo tena. Yeye habadiliki, Yeye ni Mungu. Mungu akiwahi kusema lolote, hawezi kamwe kupata wazo bora zaidi. Kumbukeni, hiyo ndiyo imani yetu. Mungu alifanya njia kwa ajili ya mwanadamu kumwabudu chini ya damu iliyomwagika huko Edeni, kamwe hajaibadilisha. Hawezi kuibadilisha. Kama aliibadilisha, amepata wazo bora kuliko alilokuwa nalo hapo mwanzo, kwa hiyo hawezi kuwa nalo. Yeye daima ni vile vile. Mungu daima aliinua, taifa ambalo lilienda kombo, akamchukua mtu na kumsimamisha huko nje na kumletea Neno la Mungu, naye akakihukumu kitu hicho chote. Akachukua kutoka hapo na kuendelea. Kamwe Yeye hatachukua dhehebu na kufanya hivyo. Atakuchukua wewe kama tu utamsikiliza Yeye, ujisalimishe mwenyewe.

71 Naam, kitu kile kile alichozaliwa ulimwenguni na kupewa nguvu kufanya, alisimama akiwa mfungwa wa kitu hicho hicho. Walimfanya awafanyie vitimbi kwa ajili ya burudani,

kuwaburudisha, vitimbi. Loo, jamani! Akamwacha mwa—mwanamke amshawishi kutoka kwenye Neno la Mungu. Neno la Mungu lilikuwa ni siri, kwake. Ilikuwa ni karama ya Kinadhiri, na haikumpasa kumwambia mtu yeyote hilo. Lakini aliuachilia ushawishi wa mwanamke.

72 Na hilo ndilo limetupata leo hii. Tumeingiza mambo kanisani mwetu ambayo hayakuwa ya Kikristo. Hakuna kanisa linaloketi likisema hakuna wanafiki katika kanisa hilo. Muundo wote umejaa wanafiki na kila namna. Hiyo ni kweli. Bali nitawapa hakikisho hili . . . Sasa, hilo ni katika chama. Huenda ukawa mwanachama wa chama cha Kimethodisti, ama chama cha Kipresbiteri, bali huwezi kuwa mwanachama wa . . .

73 Huwezi kujiunga na Kanisa. Unaweza kujiunga na chama, bali huwezi kujiunga na Kanisa. Unazaliwa ndani Yake. Basi unapozaliwa ndani ya Kanisa hilo, hakuna mnafiki ndani Yake. Kila kitu mle ndani ni safi na kitakatifu, kwa kuwa umekufa, nao uhai wako umefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, umetiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu. Ibilisi asingeweza kukupata hata afanye nini. Itambidi kupitia njia ile ile uliyopitia, na halafu angekuwa ni ndugu yako. Unaona? Kwa hiyo huwezi kufanya hivyo.

74 Bali unaweza kujiunga na kanisa kwa chochote, ili tu kupata wafuasi, maamuzi. Kama nilivyosema jana usiku, yote tunayosikia siku hizi, yanaonekana kuwa ndiyo mwito mkuu siku hizi, ni, "Wafuasi zaidi, wafuasi zaidi!" Kupiga gumzo, "Tuliwashinda!" Wanapewa zawadi kwa sababu walimleta mtu mwingine kwa ajili ya shule ya Jumapili, kubadilisha dini. Naye ni kitu gani wakati ulipomleta pale? Yeye alisikia nini? Maskini Yezebeli aliyejipaka rangi akizungumza juu ya miadi yake usiku uliotangulia, ama maandishi ma—madogo yanayoning'inia ukutani. Nanyi mnajua hiyo ni kweli. Nao Wapentekoste wakitumbukia kwa urahisi ndani yake! Mnaacha mahali fulani kuwatengenezea fasihi yenu, yale mnayofundisha.

75 Kitu kilicho juu sana kanisani ni mzee, sio askofu, sio kiongozi wa jimbo ama kitu fulani, Mungu hushughulika na mzee wa kanisa hilo. Sasa, yeye hulipa kanisa lake ujumbe wake, na yale wanayohitaji.

76 Naam, akamwacha mwanamke akamshawishi kuliacha Neno la Mungu. Ndivyo walivyofanya leo hii! Walifanyaje hilo? "Vema, sasa angalieni, nitawaambia Ndugu *Nanii.* Sasa, mwajua, hao watu huko, wanafanya *lile,* wanaangalia *hili.*" Hao sio mfano wenu!

77 Kristo ndiye Mfano wenu. Yeye alisema, "Nimewapa mfano." Acha awe Mfano wako.

78 Lile—jambo lile lile kwa makanisa. Hivyo ndivyo walivyofanya hasa, kumwacha Yezebeli, mama wa makahaba, Ufunuo 17, kufanya jambo lile lile, kumrudisha moja kwa

moja kwenye maskini mfumo ule ule, sasa amepofushwa kwa mambo ya kiroho yanayoendelea. Loo, huwazii hivyo, bali umepofushwa! Usiniambie. Unaona? Nimekuwa nikivuka huku na huko kote humu nchini kwa miaka kumi na mitano iliyopita. Umepofushwa! Mambo ya kiroho, kumwona Mungu akija na kufanya vile vile hasa alivyosema Yeye angefanya katika siku za mwisho, kasema, "Vema, nawaambia, ninaamini huenda hilo likawa ni kweli, bali ile—ile huduma nyuma yake si ya Mungu." Mungu anawezaje kuleta maji machungu na matamu kutoka kwenye chemchemi ile ile? Haipo!

79 Naam, kupofushwa kwa mambo ya kiroho na Neno la Mungu, wakarudi kwenye shimo lile lile walilotolewa. Wapentekoste walizaliwa nje ya dhehebu, na mtu akawarudisha kwenye dhehebu. Pentekoste ni ujuzi ambao dhehebu haliwezi kuvumilia, kwa sababu ni ujuzi wa kibinafsi kwa kila mtu binafsi. Hiyo ni kweli. Sasa waangalieni wamesimama, wameshindwa, kundi zima. Wahudumu, hawawezi kuwaruhusu kanisani mwao isipokuwa wana ujuzi wa seminari.

80 Moja ya huduma zetu kuu za Pentekoste, hivi majuzi, inawalazimu kuwapeleka wamishenari wao mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili kuona kama I.Q. yake ni kubwa—kubwa kutosha kuwa mmishenari, moja ya madhehebu yetu makuu, waone kama I.Q. zao ni kubwa vya kutosha. Mungu kamwe hakuwa na kitu kama hicho. Yeye alisema, "Ngojeni huko juu mpaka mtakapovikwa Uweza utokao Juu." Ndipo unapata I.Q. yako, kile kinachohitajika kufanya hivyo. Hawawachunguzi kwa kile Yesu alisema wachunguzwe kwacho. Wanawajaribu kwa dhana zao wenyewe za kiakili, I.Q. kwa mmishenari. Mungu hakusema "wape nguvu fulani za kiakili," bali alisema, "Mtapokea Nguvu zitokazo Juu!" Lakini tunaliondokea Hilo.

81 Kumbukeni, kanisa Katoliki ya Kirumi kwanza lilikuwa kanisa la kipentekoste. Hiyo ni kweli kabisa, A.D. 33. Lakini kwa kuwa akina Ricky waliingia ndani yake, wakajipenyeza mle, watu maarufu, jambo la kwanza mwajua, kwenye Baraza la Nikea, lilikubali mpango huu nao wakaunda dhehebu. Kitu hicho kikafa. Yule nabii halisi aliishi wakati wake ukaisha. Karibu miaka elfu moja, likapitia katika wakati wa giza. Hicho ndicho Mungu alichoonyesha, hukumu ya mfumo huo wote hapo mwanzo. Hiyo ni kweli.

82 Wahudumu wanapitia kwenye seminari, "Ninayo Ph.D., ama LL.D.," kabla hata hawajaweza kulihudumia kanisa; waonyeshe kadi ya ushirika. Upuuzi!

83 Nabii wa Bwana alitokeza kutokea nyikani, na hakuna mtu aliyejua mahali alipotoka wala mahali alipoenda, lakini alikuwa na BWANA ASEMA HIVI! Mungu alilithibitisha. Hakuwa katika lolote la madhehebu yao. Huo ndio mfumo wa Mungu. Hiyo ni kweli.

84 Wahudumu wa seminari, walifanya nini? Wanawake waliovalia kilimwengu, wanaovaa kaptura, kukata nywele zao, na wanaume wasio na Roho ya kutosha kukemea hiyo.

85 Mwanamume yeyote, anayemwacha mke wake kufanya hivyo, anahitaji kichapo kizuri cha Injili. Hiyo ni kweli. Anajionyesha mwenyewe hana heshima, nawe unalikubali. Mwanamume yeyote ambaye angempeleka mkewe nje mtaani, amevaa maskini suruali hizo ndefu, wanazotembea nazo hapa nje, zimebana sana ngozi iko upande wa nje, na kutembea mtaani namna hiyo, ni fedheha kabisa kwa ubinadamu. Kwangu mimi, inaonyesha ya kwamba kuna ukosefu wa kitu fulani ndani. Inaonyesha utupu.

86 Ukitaka kuonekana mrembo, chukua Matendo 2:38 kidogo, Yakobo 5:14 kidogo, yachanganye yote pamoja, Yohana 3:16 kidogo, na—na yote haya, uyachanganye yote pamoja, hayo yatakuwa ni kipodozi cha kutosha kwako.

87 Max Factors, ninaona ambapo kuna dola milioni mia moja, dola bilioni mia moja zinatumika kila mwaka kwa rangi tu za midomo ama kitu fulani, moja ya vitu hivyo; nao wamishenari hudumani, wakifa kwa njaa; nanyi mnasema, "Sisi ndio kanisa." Mbona, linanifanya nione aibu! Tunaingia katika madoido haya yote, mambo makubwa. Unafanya nini? Inaonyesha ya kwamba mmeichukua roho ya Yezebeli, tupu!

88 Nilimsikia mhudumu mmoja hivi majuzi, mtu mzuri, ninampenda kama mwanadamu, ni mfuasi wa dhehebu fulani, anaishi ng'ambo ya mto kutoka kwetu, naye alikuwa na kipindi cha redio. Ndio kwanza arudi, alikuwa akizungumza kuhusu wanawake hawa hapa wanaojipaka vitu hivi vyote vya samawati, na—na kadhalika usoni mwao.

89 Vema, niliogopeshwa nusura kufa cha kwanza nilichokiona. Nilikuwa huko Los Angeles nami nilikuwa nikimngojea Ndugu Arganbright, mfanyabiashara Mkristo. Nikamwona mwanamke akija akitembea, nikawaza, "Maskini msichana!" Mimi—mimi ni mmishenari, nimeona ukoma na nimeona tauni. Kamwe sijapata kuona kitu kama hicho. Nilitaka nimwendee na kumwuliza kama ningeweza kumwombea. Nikaja kugundua kwamba, huyu hapa mwingine anapanda juu, vile vile. Sikulaumu kwa kujaribu kuonekana nadhifu kabisa, lakini kwa kweli ifanye kibinadamu. Unaona? Hiyo ni kweli!

90 Mtu huyu alisema ya kwamba walifanya ulimwengu mrembo zaidi wakati walipotengeneza kitu hicho. Kwangu mimi, kilifanya kundi la makafiri. Na, mwanamke yeyote anayefanya hivyo, inaonyesha amepungukiwa na kitu fulani, utupu ambao unapaswa kujazwa na Kristo. Na mtu yeyote atakayemwacha mke wake kufanya kitu kama hicho, inaonyesha yeye ni mtupu pia! Na mhubiri yeyote atakayelitetea kanisani mwake, inaonyesha ana utupu pia. Pia dhehebu lolote litakalolivumilia,

inaonyesha ya kwamba wamekufa. Hiyo ni kweli. Rudini kwenye Biblia!

91 Hapo alisimama Samsoni, mhanga wa kitu kama hicho, kama mfano kwetu, mtu mashuhuri. Loo, jamani, jinsi walivyomwacha afanye hivyo! Wakati Samsoni akiyatafakari makosa yake, akayatafakari mambo aliyokuwa amefanya, na jinsi alivyomkosea Mungu. Nashangaa, hivi watu hutambua, mnaposikia Jumbe kama hizi dhidi yake? Mke aliniambia hivi majuzi, kasema baada ya . . .

92 Mtu fulani alikuwa amenikemea, kasema—kasema, aliniandikia barua, na kusema, "Billy, kwa nini usiachane na hao wanawake kuhusu nywele zao zilizokatwa, na njia zao za . . . " Kasema, "Watu wanakuamini wewe kuwa ni mwonaji. Inakupasa kuwafundisha hao wanawake jinsi ya kupata karama kubwa za kiroho, na kuachana na hilo."

93 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?" Mnaona? Mnaona? Hakika! Unawezaje kufanya hilo? Mkusanyiko kama huo wa dhambi, alama yake inaonyesha. Mtu yeyote anajua ya kwamba rangi ni alama ya ukafiri. Mimi ni mmishenari. Makafiri hujipaka rangi! Wahindi walipaka nyuso zao rangi hapa Arizona kabla hawajamjua Mungu. Wakimjua Mungu kamwe, haikubidi kuwaambia tena kulihusu, wanaiondoa. Inaonyesha wanampiga Mungu vita. Wanapoiondoa, inaonyesha wana amani na Mungu.

94 Tunajiita wenyewe taifa la Kikristo, tunawaita watu wetu Wakristo. Nilisimama huko Afrika siku moja ambako Bwana alikuwa amempa afya tena mtu aliyekuwa ameumbuka kabisa, maskini mvulana mwenye makengeza, na mambo aliyokuwa amefanya pale katika muda wa yapata dakika kumi na tano. Ndipo nikauliza, "Ni wangapi," kutoka kwa laki mbili na nusu ambao nilikuwa nikiwahubiria huko Durban, "watakaompokea Bwana Yesu?" Nao wakasimama, yapata elfu thelathini na kitu.

95 Wakasema, nilikuwa na wafasiri kumi na watano, wakasema, "Walimaanisha uponyaji wa kimwili."

96 Nikasema, "Nilimaanisha wokovu!" Nikalipitisha kwa hao wafasiri tena. Nikasema, "Wote wanaonielewa . . . " Walikuwa wamebeba sanamu ndogondogo zilizonyunyiziwa damu, hirizi, kila namna ya ushirikina, makucha ya simba. Nami nikasema, "Ninyi mnaoamini na mnataka kuachana na ushirikina wenu na kumtumikia Mungu anayeweza kumpa afya mtu huyu, aliyekuwa amesimama hapa kama mlivyomwona akifanya leo hii, na hata akarudishiwa akili yake timamu, kama unamtaka kama Mwokozi wako, onyesha uaminifu wako, vunja sanamu yako ardhini." Ilikuwa ni kama tufani ya vumbi.

97 Na pale walisimama, wanawake waliokuwa uchi wa mnyama, mbali na kipande kilichoning'inia mbele zao, kote juu ya viuno vyao kulikuwa uchi. Basi nikasema, "Inueni

mikono yenu na muombe ombi la mwenye dhambi, na kusema, ‘Mungu, nirehemu mimi, mwenye dhambi.’” Kisha nikasema, “Mahali papo hapo mnaposimama, inueni mikono yenu sasa na kuukubali ubatizo wa Kristo wa Roho. Baadhi ya wahudumu hapa watawabatiza katika ubatizo wa Kikristo.” Basi wakati walipoinua mikono yao, hao wanawake wasiojua mkono wa kuume na wa kushoto, walikuja pale wakiwa uchi wa mnyama, bali walipoondoka hata waliikunja mikono yao watoke mbele ya kundi hilo. Muda wa dakika moja pamoja na Yesu Kristo uliwafanya wajue walikuwa uchi.

98 Na leo hii, mwaka baada ya mwaka, tunavua nyingi zaidi na kutoa nyingi zaidi. Na, loo, kamwe mimi . . . Na halafu tunaiita Mungu? Ni kitu gani kilicholisababisha hilo? Madhehebu yenu yanayowaruhusu kulifanya. Hiyo ni kweli. Mfumo ambao mliinuliwa kujitakasa muuache, mliurudisha moja kwa moja tena. Natumaini sisikiki wa kukufuru, natumaini mimi . . . Sio kukufuru, ni Neno la Bwana. Hakika, ndilo!

99 Sasa, sasa tunaona ya kwamba wakati Samsoni aliposimama pale akiliangalia kosa lake, akiangalia yale yaliyokuwa yamefanywa, katika dhamira yake ya ndani, kwamba alikuwa—alikuwa amemkosea Mungu, alikuwa amewakosea watu wa Mungu. Naye hapo amesimama kama mfano, akitafakari vile alivyokuwa na kutafakari sasa yale aliyokuwa. Basi alipofanya hivyo, alipaza sauti!

100 Loo, kama kanisa, usiku wa leo, lingesimama kimya kwa dakika moja na kuangalia nyuma kwenye siku ya Pentekoste, liangalie nyuma mahali tulipoanzia, na kutambua hali ambayo kanuni zetu za imani na mizozano imetufikisha. Paza sauti tena! Samsoni alipaza sauti, “Bwana Mungu, nilipizie kisasi kwa ajili ya macho yangu mawili!” Kama tungeweza kulia kilio hicho hicho cha toba, “Bwana Mungu, vitu hivi vimeniongoza kipofu nyakati hizi zote!” Alijua kulikuwako na gharama ya kulipa. Mnajua hilo sasa.

101 Meda, mke wangu, aliniambia, akasema, “Unarudi kote katika mataifa, huku na huku wakati wote, ukihubiri, unarudi moja kwa moja, watu wanafanya jambo lile lile. Basi inafaidi nini?”

102 Nikasema, “Kwenye siku ya hukumu, kutakuwako na kanda iliyorekodiwa kwenye kanda kuu ya Mungu.” Sio kwamba hamyajui mambo haya. Mungu atayafyatulia Hayo kote angani. Hana budi kuwa na Sauti kule kuuhukumu ulimwengu kwayo, nayo Sauti hiyo ni Injili.

103 “Nilipizie kisasi, Bwana, kwa adui zangu. Yalipizie kisasi macho yangu! Waliyang’oa, Bwana, nami huyu hapa nimesimama.” Samsoni pia alijua ya kwamba kulikuwako na uwezekano ya kwamba huenda Mungu mara nyingine tena akamsikia. Hata katika hali zake, kulikuwako na uwezekano.

Loo, enyi kanisa, kuna uwezekano bila kujali yote wanayofanya. Kama tunavyosikia leo hii, sana sana, "Wengi sana walifanya maamuzi, maamuzi." *Maamuzi* linamaanisha "jiwe, kukiri." Kama nilivyosema awali, jiwe lina faida gani ikiwa huna mwashi pale aliye na Neno kali kulikata jiwe hilo likawa jiwe lililowekwa kwa ajili ya jengo? Inafaa nini kufanya maamuzi ikiwa mngali mtawaacha wanawake na wanaume wabaki jinsi walivyokuwa, na kujiunga tu na kanisa? Ni lundo la mawe yasiyochongwa kuwa chochote. Tunachohitaji ni mwashi, mtu aliye na Neno la Mungu, nguvu zilizohakikishwa kuthibitisha ya kwamba Mungu alimtuma, kulichonga Kanisa hilo na kukatilia mbali mambo ya kilimwengu, na kuyachonga yawe mawe ya wana na binti za Mungu wanaoingia katika jengo Lake. Kweli kabisa. Loo, jamani!

104 Yeye alijua uwezekano, hata hivyo, ya kwamba kunaweza kuwako na Mungu ambaye angeyasikia maombi. Laiti tungalifanya tu hivyo usiku wa leo! Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, ninii... Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Yesu alisema, ama Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, ambayo ilinukuliwa muda mfupi uliopita, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Nasi tunaita maisha haya ya kimadhehebu yaliyo ndani yetu Uzima wa Kristo, na kufanya mambo tunayofanya? "Kwa nini kuniita 'Bwana,' na hamzitii amri Zangu?" Mnaona? "Kwa nini kuniita hivyo?"

105 Loo, kama huna washiriki watano kanisani mwako, pata Ukweli wake, uwezekano. Na vile vile sasa, uwezekano. Lakini hao wa siku hizi hawaonekani kushika ono kama vile Samsoni alivyolishika. Hawaonekani kulipata, wanawazia, "Vema, mimi nimetulia vizuri sana, nasi tuna makanisa mazuri, wala hatuna ninii..." Mnaona?

106 Biblia ilisema, "Wakati huo wa kanisa tajiri la Laodikia, wasingekuwa na haja ya kitu, na wasijue ya kwamba wao ni uchi, vipofu, wenye mashaka, na hata hawajui hilo." Sasa, kama ungalimwona mtu akishuka barabarani, aliyekuwa uchi na kipofu, nawe ungeweza kuwaambia kwamba walikuwa katika hali hiyo, walikuwa uchi, iliwabidi waingie mahali fulani na kujificha, vema, kuna uwezekano ya kwamba ungeweza kumwondosha huyo mtu barabarani. Lakini wakati wanapogeuka, pasipo na nguvu za kiakili za kutosha kujua hilo; bali sasa kanisa halina nguvu za kiroho za kutosha kujua hilo. Uchi, mnyonge, kipofu, mwenye mashaka, maskini. Kristo akiwa nje, akibisha, akijaribu kuingia ndani, na hata hivyo mnasema hamna haja ya kitu.

107 Ninajua hilo ni la kigeni kwa baadhi yenu, bali ni Ukweli wa Mungu. Neno linasema hivyo. Hawashiki ono. Unaweza kuwaambia kulihusu, linawaruka tu. Labda papo hapo pana imani ndogo, kesho yake Hiyo yote imesahaulika, wanarudi moja

kwa moja kwenye karamu yao ya kadi, na shona na kufuma yao yote, na—na kuwa wafuasi wa vitu hivi vyote, na Hiyo yote imesahaulika kabisa.

108 Mungu anaweza kumfanyia mtu kitu fulani, na, "Loo, vema, kilitukia tu." Mnaona, ibilisi amezitia nia zao sumu sana kwa mambo haya, hata hawajui mahali walipo wenyewe. Wanakaa kimya! Loo, wanaweza kupiga makofi yao, na kupaza sauti "amina," wakacheza katika Roho. Hilo halimaanishi kitu chochote. Nimewaona makafiri wakifanya hivyo. Hiyo ni kweli. Wanafanya mikutano mikubwa, loo, mnasema, "Sisi tungali tuna uamsho, Ndugu Branham." A-ha, ni uamsho wa aina gani? Mna mikusanyiko ya kanisa.

109 Ilikuwa ni huko chini Kentucky, tulikuwa tunaiita, "Mikutano iliyorefushwa," na hivyo ndivyo karibu ifanyavyo, kukawilishwa. Nao wako mbali sana na kuvutiwa kwa Injili. Hiyo ni kweli. Naam, wanasema, "Loo, tulikuwa na mkutano. Mwajua nini? Tulimwalika Daktari *Fulani-wa-fulani* kuja mjini, nasi tulikuwa na maelfu. Makanisa yote yalishirikiana." Tulifanya nini, tulipokuwa na uamsho? Tuliwarejesha watu kwenye Neno la Mungu, kisha Mungu akaanza kutenda kazi kanisani? Tulifanya nini? Tuna kundi la kukusanyika pamoja, na kumetameta kwa mapambo ya kilimwengu, hiyo ni kweli kabisa, utaalamu, maonyesho ya Hollywood.

Loo, mnasema, "Hao ni Wabaptisti."

110 Hao ni Wapentekoste. Kweli! Huko juu jukwaani, wanawake wakirukaruka na kucheza, na kuonekana wabaya sana, wamevaa maskini nguo zilizobana, ambazo, ni aibu. Siwezi hata kupata maneno sasa hivi. Ni aibu. Wanaume wameketi pale, wakipiga makelele, "Utukufu kwa Mungu! Haleluya!" Ni roho ya aina gani mliyo nayo, hata hivyo? Mnafikiri Yesu angekishangilia kitu kama hicho? Yeye angekihukumu! Mnafikiri Isaya angalijitokeza jukwaani, Yeremia, Amosi, mmoja wa hao manabii wa Agano la Kale ajitokeze jukwaani kama walivyofanya, na kuona mambo waliyoyaona yakiendelea, jinsi waliyakemea, kasema, "Mungu yeye yule mnayedai kumtumikia atawaangamiza." Angesema jambo lile lile leo hii. Hakika angesema!

111 Hilo halimaanishi kitu, maonyesho. Tuna Hollywood chungu nzima, bali haishushi Roho na nguvu za Mungu. Huenda ikaleta shauku, bali haileti nguvu za Mungu.

112 Hawako tayari kulipa gharama. Samsoni aliomba vizuri. Aliomba nini? Katika kufunga, huenda nikasema hivi. "Bwana, hebu nife pamoja na adui." Hiyo ndiyo shida, hawataki kulipa gharama ya kufa. Umejichochea ukaingia katika jamii fulani, katika kundi la watu unaoshirikiana nao na kucheza karata, kukaa nyumbani na kuangalia vipindi, kula chipsi za "tata" na kunywa Koka. Kanisa liko tupu. Hiyo ni kweli. Wanakufanya

utie sahihi kadi, utahudhuria shule ya Jumapili miezi sita katika mwaka. Shauku kama hizo za kubuniwa na wanadamu! Unachohitaji ni Roho Mtakatifu. Loo, unasema, "Ninaye." Hakika hutendi kana kwamba unaye. Naam, bwana. Acha mhubiri ahubiri saa moja ama kitu kama hicho, uko tayari kuita halmashauri ya wadhamini na kumtupa nje. Hiyo ni kweli. Loo, u—unataka kula keki yako na kuihifadhi vile vile. Huwezi kufanya hivyo. La, bwana. Huna budi kujisalimisha. Una gharama ya kulipa. Una utakaso wa kufanya. Nami nawaambia, kanisa lote ulimwenguni linahitaji kusafishwa kote tangu mimbarani hadi kwenye chumba cha bawabu. Hiyo ni kweli. Ni Kweli. Hawako tayari kugharamia.

113 Lakini Samsoni aliomba vizuri wakati aliposema, "Bwana, acha nife pamoja na hawa Wafilisti." Alikuwa ameshindwa, lakini, "Acha nife." Huna budi kuwa tayari kufa kwa adui ambaye amepata ushindi huu juu yako. Huna budi kuwa tayari kusalimisha mawazo yako mwenyewe. Samsoni alikuwa tayari kulipa gharama apate—apate nguvu za Mungu tena.

114 Sijui kama ninyi wanawake mko tayari kuachilia nywele zenu zikue? Sijui kama wewe mwanaume una ujasiri wa kutosha kumwambia hivyo? Unapaswa kuwa kichwa cha nyumba. Yeye mwanamke ni shingo, anakugeuza. Hilo ni kinyume! Mnafikiri uamsho wa kutikisa ungeweza kamwe kuwaondoa wanawake hawa kutoka kwenye ofisi za umma, polisi barabarani na kadhalika? Anapaswa kuwa jikoni. Mnafikiri mngeweza kumrudisha huko tena? La, bwana. Kamwe hatafanya hivyo, isipokuwa aokoke, ndipo atafanya hivyo. Haitakubidi kumwambia lolote juu yake, yeye atapata mahali pake, Roho Mtakatifu atamwongoza kwenye mahali pake. Lakini kusema, "Roho Mtakatifu ananiongoza"? Kwenye hilo lililo kinyume na Neno? Usimwite huyo Roho Mtakatifu.

115 Uko tayari kulipa gharama? Hiyo ni katika ninii. . . kanisa la Kipentekoste, mko tayari kulipa gharama? Na jambo ndilo hilo. Mnaona tunasimama katika aibu ya jinsi gani. Vema. Samsoni, akiwa tayari kulipa gharama apate nguvu za Mungu tena. Loo, ninasikia baadhi yenu mkisema, "Tuna uamsho, hata hivyo, Ndugu Branham." Lakini mnapata nini baada ya kupata uamsho?

116 Billy Graham alisema katika ujumbe wake, Louisville, Kentucky, wakati nilipoketi kwenye, pamoja naye kwenye kiamshakinywa, alisimama kule, akaichukua Biblia na kusema, "Biblia hii ndiyo njia ya Mungu ya kufanya mambo." Jinsi hilo lilivyo kweli! Lakini basi fanyeni hilo, ndilo jambo linalofuata. Akasema, "Paulo aliingia mjini na akapata mwongofu mmoja, akamwacha huyo mwongofu kule, mwongofu mmoja katika mji fulani. Mwaka uliofuata akarudi, naye mwongofu huyo alikuwa na thelathini ama arobaini walioongoka, na kuletwa katika Kristo." Akasema, "Ninaingia mjini, nami nafanya nini,

napata waongofu elfu thelathini, maamuzi." Kasema, "Narudi katika mwaka mmoja, sina thelathini." Akasema, "Kuna shida gani?" Ndipo akawakabili wahubiri, kasema, "Ni ninyi wahubiri wazembe, mnaoketi mmeweka miguu yenu juu ya dawati na hamwendi kuwatembelea watu."

117 Sasa, huo ulikuwa ni ukweli mwingi sana katika hilo, hiyo ni kweli, bali haukuwa ni kweli yote. Kama yule mtu aliyekuwa akila tikitimaji, akasema, akampa aume kidogo, maskini mzee mweusi, naye akasema, "Loo, hiyo ilikuwa ni tamu, bali yapo zaidi." Na hiyo ni kweli.

118 Basi mambo yalikuwa hivi. Mimi nilikuwa ni nani kumwambia mwinjilisti huyo mashuhuri, mimi nilikuwa ni nani kusema neno kwa mtu kama Billy Graham? Na iwe mbali nami. Huyo ni mtumishi wa Mungu. Nisingelizungumzia isipokuwa yeye aniulize, ndipo labda ningeweza kusema jambo fulani. Bali ningalitaka kusema hivi, "Billy, ni mhubiri gani mzembe aliyeweka miguu yake juu ya dawati juu ya wongofu wa Paulo, yule aliyempata? Hapakuwapo na mhubiri nchini. Ilikuwa ni kitu gani? Paulo hakumwacha kwenye uamuzi. Wakati alipofanya uamuzi wake, alisimama hapo pamoja na Neno la Mungu na kumchonga akawa mwana wa Mungu, ndipo usingeweza kumnyamazisha."

119 Hiyo ndiyo shida leo hii, maamuzi haya yote yanapaswa kuchongwa yawe wana na binti za Mungu. Jitakaseni, mkarejee kwenye Neno na kurejea kwenye Injili. Hakika, hilo ndilo tunalohitaji. Naam, tunao uamsho siku hizi, bali ni kitu gani? Ni uamsho wa kimadhehebu. Baptisti ilikuwa na msemo, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Mlipata nini? Nilikuwa kwenye kanisa ambapo walikuwa na uamsho, walisema, nao iliwabidi kufumukana watoe kipumziko cha dakika kumi na tano, watu wapate kutoka nje na kuvuta sigara katikati ya shule ya Jumapili na huo. Na, mchungaji alivuta sigara, pia. Biblia ilisema, "Jitakaseni na tabia zote chafu." Mnaona? Sasa tutafanya nini juu ya jambo hilo?

120 Vema, mnasema, "Si sawa." Roho Mtakatifu, ajapo, Yeye atawafundisha mambo haya yote. Mnaona, hakika alifanya hivyo.

121 Ndipo mtu fulani akasema jambo fulani kuhusu uponyaji wa Kiungu, nao wakadai, "Ilikuwa katika siku nyingine." Mnaona, wakielekeza kwa yale yaliyokuwako. "Labda itakuwa huko katika Utawala wa Miaka Elfu." Unahitaji uponyaji wa Kiungu wa nini kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati hupatikani na mauti? Leo ndiyo siku! Hii ndiyo siku.

122 Unasema, "Vema, tuna miamsho." Angalieni utovu wa uadilifu kanisani. Angalieni jinsi linavyopotoka kila mwaka. Yaangalieni makundi yetu ya Kipentekoste, jinsi yalivyoanguka. Fungeni macho yenu na muwazie juu yake miaka kumi na

mitano iliyopita wakati nilipokuwa hapa, kisha mwangalie yale mliyo nayo siku hizi. Mnajua hiyo ni kweli! Ni dhambi na aibu. Hiyo ni kweli. Mnaenda mbali zaidi na zaidi kutoka kwenye Neno la Mungu, wakati wote.

123 Samsoni alijua hali zake za kurudi nyuma. Alijua asingepata nguvu kukabiliana na changamoto ya saa hiyo, ingawa alikuwa hapo. Mitambo yake yote ilikuwa hapo. Misuli ile ile ambayo ingechukua mfupa wa taya na kupiga na kuwaangusha Wafilisti milioni moja, misuli ile ile ilining'inia juu ya mtu yule yule. Mabega yale yale ambayo yangeweza kubeba malango ya Gaza kuyapeleka juu ya mlima, ilikuwa ingali ni misuli ile ile iliyoning'inia juu yake. Loo, ningesema jambo fulani hapa, mnaona. Lakini yeye alijua ya kwamba asingeweza kukabiliana na changamoto ya saa hiyo.

124 Vivyo hivyo kanisa linajua, katika utovu wake wa uadilifu, kamwe hatutakabiliana na changamoto ya wakati huu. Ukomunisti unakichukua kitu hicho chote. Nasi tunajaribu kufanya nini? Kupata faraja, kwa kujiunga, kujifunga nira pamoja na watu hawa, madhehebu ambayo hata hayaamini katika uponyaji wa Kiungu na nguvu za Mungu. Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokubaliana? Tunajifunga nira miongoni mwa upuuzi kama huo, na kisha tumtarajie Mungu. . . Tunasema, "Idadi kubwa." Mungu haoni idadi kubwa. Mungu huangalia tabia.

125 Nilisema Elieza alitoa jasho mpaka akapata tabia katika Rebeka. Ndipo ilimbidi kumvalisha nguo, kumfanya tayari, kumfanya asimame kimya na kuusikiliza Ujumbe wake. Shida yake ni kwamba, siku hizi, unapoipata tabia, ni vigumu kuwafanya wasimame kimya muda mrefu vya kutosha kuvaa nguo na kujivika. Hiyo ni kweli. Maskini Ricky fulani tayari amewavuta akawaelekeza kwingine. Hiyo ni kweli. Lakini, pale, Elieza alitokwa jasho.

126 Sasa, Samsoni alijua ya kwamba hakuwa na nguvu, ingawa alikuwa na misuli. Nasi tuna mitambo yetu yote. Tunao wakuu wa wilaya, tunao maaskofu wote, tunao maaskofu wakuu, tunao mapapa, tunao mfumo wa uongozi msonge. Tuna utaratibu wote. Tuna ujenzi mkuu, mijengo mikubwa mno na karibu pesa zote za duniani. Zinatufaa nini? Ni shaba iliayo na upatu uvumao. Hiyo ni kweli. Lakini tunajua hatuwezi kukabiliana na changamoto ya wakati huu.

127 Leo hii, katika Urusi, Ukomunisti unauchukua ulimwengu. Kuna shida gani? Ni mtu aliye na ujasiri wa kusimama chini ya imani, ingawa si ya kweli. Ukomunisti ni asilimia moja tu ya Urusi, asilimia moja! Asilimia tisini na tisa ingali ni ule unaoitwa Ukristo, huru, bali hawana I.Q. ya Injili. Hawana kinachohitajika, ingawa wanazo pesa na wana haya yote, bali hawana ule ujasiri na neema. Kile Mungu anachohitaji katika

Urusi ni mtu mmoja aliyepakwa mafuta kwa nguvu za Mungu, pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu.

128 Samsoni alijua alichohitaji. Huenda tukaigeuza Marekani nzima, na kila mmoja wao aende kanisani, bado hatujalipata. Tuna. . .hatuna kile kinachohitajika. Wale wanafunzi hawakuwa nacho mpaka walipoenda kwenye Pentekoste. Yesu aliwaambia hawakuwa na Hicho, baada ya kuwa wakihubiri kwa miaka mitatu. Wangali walikihitaji. Kanisa linakihitaji. Hiyo ni kweli.

129 Angalieni, Samsoni alijua ya kwamba yeye alikuwa mhitaji, hakujitosheleza. Madhehebu hayawezi kukileta Hicho. Hayalithibitishi Neno, wanafundisha dhidi Yake. Naam. Mwajua, lakini Samsoni akitambua hilo, ya kwamba hakujitosheleza mwenyewe, ingawa alikuwa na mfumo wake wote, angali hakujitosheleza. Mwangalieni! Wafilisiti wakijigamba juu ya ushindi wao. Kamwe hawakumwona akikiinua kichwa chake juu, midomo yake ikisonga huku na huku katika maombi, machozi yakitiririka kutoka kwenye yale mashimo ambamo wakati mmoja alikuwa na macho ndani yake. Hawakuona hilo. Walininii tu. . .walikuwa na wakati mzuri mno. Yeye alimtaka Mungu ajidhihirishe Mwenyewe tena kwa Yezebeli huyu. Loo, laiti tungalikuwa na Samsoni wengine kuinuka! Loo, enyi kanisa! Sio dhehebu jipya, kuanzisha kanuni nyingine ya imani ama mvua ya vuli. Tunahitaji nguvu za Mungu. Hiyo ni kweli.

130 Alijua kile kingetukia kama Mungu kwa vyovyote angejibu maombi yake, bali alikuwa tayari kukabiliana na jambo hilo. Alikuwa na bidii kabisa. Loo, laiti kanisa, usiku wa leo, lingesimama tu katika hali hiyo, lenye bidii sana, mkijua ya kwamba hamna budi kusalimisha kila kitu mnachokithamini katika ulimwengu huu. Kama wanaume na wanawake wako tayari usiku wa leo kujua ya kwamba itawatenganisha na kila kitu cha ulimwenguni. Wahudumu, wataacha kukupapasa mgongoni na kukwambia, "Daktari *Fulani-wa-fulani,* ilikuwa ni vizuri sana, hivi utaenda kuogelea pamoja nasi alasiri ya leo?" Ondoeni michezo ya banko kanisani, na mashindano ya mbio, na karibu bahati nasibu. Banko ni bahati nasibu. Na milo hii yote ya supu mpate kumlipa mhubiri; rudini kwenye mfumo wa Mungu wa kutoa zaka! Rudini kwenye Neno! Wako tayari kufanya hivyo? La, bwana, hawakuwa. Mnajua inagharimu nini. Mwanamke huyo atakuita wa mtindo wa kale tena. Mungu atakuita mwenye heri.

131 Uko tayari kufa? Hiyo ndiyo shida yake, unataka kuwa hai kwa Hollywood, wakati uo huo kuwa hai pamoja na Mungu. Hazitachanganyikana. Mbegu, Yesu alisema, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, inakaa peke yake." Kamwe hutazalisha chochote.

132 Loo, enyi kanisa la Jesus Name! Ni kanisa tukufu jinsi gani, ni Jina tukufu jinsi gani, Jina la Yesu! Mko tayari kufa? Ninyi Assemblies of God, General Assembly, mko tayari kufa? Methodisti, Baptisti, Presbiteri, mko tayari kufa kwa adui wenu? Mko tayari kulipa gharama ya kujitolea, kweli, kwa uaminifu? Sio tu kuja na kusema, "Vema, nitajaribu nione jinsi itakavyotokea." Hujawa tayari bado. Huna budi kuwa tayari kulipa gharama, kisha ufe.

133 Ninyi akina baba, ninyi akina mama, mko tayari kuweka madhabahu nyumbani mwenu, na kuiondolea mbali hiyo televisheni? Mko tayari kuondolea mbali jozi hiyo ya karata kutoka mezani? Hivyo vitabu vya kilimwengu ambavyo watoto wenu wanavisoma, vinavyoandaa maskini bongo zao kwa ajili ya mlipuko ambao ibilisi atawapa. Mko tayari kuweka madhabahu ya kale ya familia tena? Ama mnataka tu kuendelea jinsi mlivyo? Mnataka kuendelea, hamko katika hali ya kuja bado; bali ninaomba ya kwamba ninyi ni kama Samsoni, mnaiona gharama na mko tayari, "Bwana, jalia nife pamoja nao."

134 Yeye alijua, kama Mungu akiyajibu maombi yake, kile yatakachomgharimu. Watu wengi, nimewaona moja kwa moja tangu nimekuwa hapa, wanakuja madhabahuni na Roho Mtakatifu anakuja juu yao, nao hawataki kufa. Wanataka kubakia hai ulimwenguni. Huwezi kuwatumikia miungu wawili wakati ule ule. Uko tayari kuachana na kila kitu, kumtumikia Mungu? Msikilizeni akilia, "Bwana, mara hii tu tena!"

135 Hivi kanisa la Kipentekoste, Halmashauri Kuu, Assemblies of God, church of God, ninyi wengine wote, mko tayari kulipa gharama? Mko tayari kusema, "Mara nyingine, Bwana! Mimi hapa nimesimama. Sikuwa na ujasiri, ile roho yenyewe ya Kikristo kupeana mikono na ndugu yangu wa umoja, ama ndugu yangu wa utatu. Sikuwa na ujasiri wa kufanya hivyo. Sikuwa na neema ya kufanya hivyo, ninapoona mahali imenifikisha, kuvunjika katika madhehebu na kuondolewa kwenye ushirika, pamoja na kusanyiko lililotiwa sumu sana mmoja dhidi ya mwingine hata wanazungumza mmoja na mwingine kwa nadra mtaani, wakati, sisi tumefinyangwa katika udongo mmoja, kwa Roho Mtakatifu"?

136 Uko tayari kupaza sauti, "Mara nyingine, Bwana, jalia litukie"? Kama uko tayari, Mungu hakika atayasikia maombi yako. Angalieni wakati mtu huyo, pamoja na umbile hilo lote lililosimama hapo, mfumo wake mkubwa, bali alikuwa angali kipofu. Alijua gharama yake, alijua ule uwezekano, naye akasema, "Mara nyingine, Bwana! Mara nyingine nilipizie kisasi kwa ajili ya macho yangu!" Wakati alipofanya ombi hilo, Mungu alilijibu. Kila mshipa wa mwili wake ukaanza kukazika, Roho akaanza kuingia kwenye misuli hiyo. Loo, laiti tungalikuwa na Roho ambaye huja kwenye mkutano wetu wa maombi ya Jumatano usiku, kwenye shule yetu ya Jumapili, tusikie umbile

la misuli ya nguvu za Mungu likikaza, ambamo Roho Mtakatifu anaweza kuingia. Sio katika dhihaka, bali katika Roho wa kweli kufunua siri ya moyo na kuweka sawa dhambi iliyomo, aondoe uovu.

137 Wakati mishipa yake ilipoanza kukaza, "Hebu nife pamoja nao! Nilizaliwa nipate kuwaangamiza, jalia nife pamoja nao." Ndipo mishipa yake, misuli yake ikakazika, misuli yake mikubwa mno ikapata nguvu, Roho Mtakatifu akaanza kutenda kazi juu yake, ndipo akalipinda jiwe hilo kwa nguvu zake kuu, nalo likaporomoka. Yote tunayohitaji ni maombi maaminifu, "Mara nyingine tena, Bwana!"

138 Wakati tunapopaswa kuwa katika Nchi ya Ahadi, tungali tunatangatanga nyikani. Kama vile Israeli, walivyotaka torati, jambo fulani wangaliweza kufanya. Huwezi kufanya lolote kulihusu. Mkubali Kristo! Tulitaka fundisho, kitu ambacho tungeweza kujigamba kwacho, na kupata tabaka tofauti la watu kutoka kwa jamaa huyo mwingine. Mnaona mahali tulipofikia? Tumepofushwa. Vema.

139 Hilo dhehebu kubwa likaporomoka. Sikuzote imekuwa hivyo wakati Mungu anapoingia, vitu hivyo vingine huporomoka. Ndipo ukaja ushindi mkuu kuliko wote wa Samsoni. Loo, laiti ningaliweza kuliona Kanisa la Mungu aliye hai limesimama usiku wa leo, "Mara nyingine, Bwana! Mara nyingine, tutumie uamsho, hata ukinigharimu kila kitu. Kama ukigharimu kila kitu nilicho nacho, nitumie uamsho. Utume juu yangu, Bwana." Lisikie kundi hili la karibu watu mia tatu, ama zaidi, hapa usiku wa leo, likilia kwa sauti moja, "Bwana Mungu, mara nyingine tena jalia nimwone Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Jalia nijue ya kwamba Yeye yuko karibu nami. Jalia nijue ya kwamba Yeye yupo hapa kunishughulikia mimi. Niko tayari sasa."

140 Loo, walitolewa, adui wote aliangamizwa. Wapentekoste wanasimama kwenye nguzo hiyo usiku wa leo. Vitu ambavyo mlizaliwa mpate kuviangamiza, vimewashinda. Tubuni, iteni kwa sauti kuu, "Bwana, mara nyingine tena, mara nyingine tena jalia tulione!"

141 Hebu niseme hili, rafiki yangu. Afadhali umwangamize adui wako kabla adui wako hajakuangamiza. Irudisheni ile mikutano ya maombi ya mtindo wa kale. Toba ya mtindo wa kale, wakati walipokaa madhabahuni mpaka wakafa na kumalizana na dhambi. Kamwe hujawahi kumwona mwanamke akienda madhabahuni na kuifia dhambi, halafu kesho yake anarudi akiwa na nywele zilizokatwa, rangi usoni mwake. Hakuna kitu kama hicho. Roho Mtakatifu hufundisha, maumbile hufundisha, tabia ya Roho Mtakatifu. Hamjawahi kamwe kuona wanawake wakitoka nje na kuvaa kizinifu; waingie na kujaribu kujifunika. Hamjawahi kamwe kumwona

mwanamume aliyeogopa kusimama na anaogopa maskini mke wake atamwacha ama kitu kingine, kwa sababu alichukua hatua. Vema, wanaume walikuwa ni wanaume siku hizo. Walinena, walikuwa ni wanaume, walitawala nyumba yao. Walikuwa ndio kichwa cha nyumba. Lakini Marekani hii ya ndoto. . .

142 Ndio kwanza nijulishwe na maskini mwanachuoni wa Kiyunani, anayeketi hapa akiniangalia sasa, aliyetoka Uyunani, mwanachuoni katika Kiyunani, naye alianza kucheza kanda zangu na akaangalia Ujumbe. Kasema, "Ninajua ya kwamba hata huna elimu, bali, Ndugu Branham, Maneno yako na Ujumbe wako unaendana kikamilifu na fasiri ya Kiyunani ya Biblia." Kasema, "Ni sahihi kabisa. Uliyosema ni sahihi kabisa." Naye akanijia, alikuwa akiniambia, "*Laodikia* linamaanisha 'mwanamke' katika Kiyunani." Huu ni ulimwengu wa wanawake, ni kanisa la wanawake, ni wakati wa wanawake. Kasema, "Vema, wanaume hawatafanya hilo." Ni lini Mungu aliwahi kamwe kuingia katika hali hiyo? Naam, mko tayari kurejesha uamsho? Mko tayari?

143 Mwanamke alisema, "Ninayo haki ya kufanya yale nitakayo. Hayo ni majaliwa yangu ya Marekani." Ni majaliwa yako ya Kimarekani, si majaliwa yako uliyopewa na Mungu, hata hivyo. Kondoo. . .Mbuzi sikuzote ataanzisha vurugu, bali kondoo husimama kimya na kuachilia haki zake. Mnaona? Ikiwa wewe ni mtoto halisi wa Mungu, utaachilia haki zako za Kimarekani kwa Roho Mtakatifu na kumwacha akufinyange na kukufanya jinsi unavyopaswa kuwa. "Mara nyingine tena, Bwana." Loo, jamani!

144 Loo, kanisa, achaneni na Delila wa Hollywood, atawaua. Anausonga uhai wa kiroho kutoka kwenu. Achaneni naye! Maonyesho yenu ya Hollywood jukwaani, Hollywood yenu, mapambo yenu, mkutano wetu hauna budi kuwa hivi kwamba utakuwa katika mahali pakubwa kama walimwengu wengine, hauna budi kuwa katika makanisa yaliyo makubwa kuliko yote. Mwinjilisti akija mjini, inawabidi kumuahidi kiasi fulani cha pesa la sivyo hatakuja. Ni fedheha jinsi gani! Inaonyesha mahali hazina yako ilipo, moyo wako uko huko. Mgeukieni Mungu kwa mioyo yenu yote na kwa Neno Lake, na hebu tupaze sauti, "Mara nyingine tena, Bwana! Mara nyingine tena, tuonyeshe Uwepo Wako!"

145 Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu," huo ni kosmosi, ninaamini hapo, ndugu, "utaratibu wa ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona," mwaminio, "kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Zaidi ya hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya." Si anayejifanya kuamini; bali aaminiye. Loo, kanisa, sisi. . .Yesu

hajafa, Yeye amefufuka katika wafu. Yeye yupo papa hapa sasa. Kama sikuwa na msaada huo, nisingesema yale nisemayo. Nami najua Yeye yupo hapa. Naye anajithibitisha Mwenyewe hapa. Daima Yeye yupo hapa kulithibitisha Neno Lake. Kama alisimama hapa usiku wa leo, Yeye angesema nini? Angerejea moja kwa moja kwenye Neno tena, akisema jambo lile lile ambalo Yeye alisema.

146 Sasa, mnasema, "Huyo alikuwa ni Yesu akizungumza?" Vema, kama haikuwa hivyo, hakika nisingetaka kusema hilo. Bila shaka! "Inaweza kuthibitishwaje?" Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja.

147 Baba wa Mbinguni, watumishi Wako wanaweza kusema yote wanayotaka kusema, nasi tunaweza kuuleta Ukweli dhahiri sana kwa watu, bali hata hivyo ungali tu ni mhemko. Bado ni midomo tu ya mwanadamu ikilihubiria kusanyiko. Basi, Bwana, Wewe ni wa Kimbinguni. Na popote ulipo, kuna ishara za Kimbinguni, kuna miujiza inayotendeka, mambo yasiyoweza kuelezeka. Ulipokuwa hapa duniani, Wewe ulitembea huku na huku miongoni mwa watu, ukawaponya wagonjwa. Mwanamke aliligusa vazi Lako wakati mmoja, na Wewe ukageuka, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Hukujua, Wewe Mwenyewe. "Ni nani aliyenigusa?" Lakini Mungu aliyekuwa ndani Yako, Wewe uliijua siri ya moyo, kwa sababu Biblia inasema, "Neno la Mungu lina nguvu na ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo ya moyo." Na Wewe uliangalia chini, maskini huyo mwanamke asingeweza kujificha, na Wewe ukamwambia imani yake ilikuwa imemwokoa.

148 Wewe ulisema, "Sitendi lolote mpaka Baba anionyeshe kwanza. Baba anatenda kazi, nami nafanya kazi vile vile." Kama ungalikuwa hapa usiku wa leo, Wewe ungefanya jinsi tu Baba alivyokuonyesha kufanya.

149 Nami naomba, Bwana, ya kwamba unaweza kulileta kanisa hili mara nyingine tena, Bwana Mungu, watu hawa waliojumuika hapa usiku wa leo kutoka makanisa yote mbalimbali, Methodisti, Baptisti, Katoliki, Presbiteri, Wapentekoste, na kila namna ya chapa zilizo juu yao. Wewe huangalii chapa, unaangalia kitambulisho cha Damu. Naomba, Baba wa Mbinguni, kwamba usiku wa leo, ya kwamba hawa watu hawatajali chapa waliyovaa, na ikumbukwe Pentekoste sio dhehebu, ni ujuzi unaomjia mwanamume yeyote ama mwanamke atakayekutumainia Wewe. Waponye wagonjwa, Bwana, waokoe waliopotea. Jitwalie Mwenyewe heshima.

150 Sasa nawakabidhi wasikilizaji hawa, pamoja na maneno haya yaliyokatikatika, Bwana. Mimi si mnenaji hodari, mimi sikidhi viwango vya kulileta Neno, bali ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu atayachukua mambo haya na kuyafunua na kuyafanya yajulikane kwa ule mtazamo yaliyotolewa nao. Sio

kujisikia duni, bali kujisikia mnyenyekevu sana. Sio kuwa tofauti, bali kuwa mkweli na mwaminifu kwa watu, kama vile ningekuwa kwa Mungu. Kwa kuwa ikiwa siwezi kuwa mwaminifu kwa watoto Wake, ninawezaje kuwa mwaminifu Kwake?

151 Nami naomba, Mungu, ya kwamba Wewe utalithibitisha Hili—usiku wa leo, moja kwa moja mbele za watu sasa, ili waweze kujua ya kwamba wanaishi katika vivuli vya wakati, ya kwamba Ujumbe wa wakati huu ni "kutubu na kuigeukia ile Imani ya baba zetu." Tujalie. Nami ninalikabidhi Kwako. Waokoe wenye dhambi. Wajaze waaminio. Waponye wagonjwa. Ulete Utukufu. Pia jalia sote tupaze sauti kwa moyo mmoja, "Mara nyingine tena, Bwana, mara nyingine tena!" Jalia iwe mara nyingine tena! Tunaomba katika Jina la Yesu.

152 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kwa njia ya maombi, hivi huwezi kutafakari hili, "Ni mimi, Bwana? Nifanyeje, ya—yanipasa kufanya nini?" Jichunguze tu mwenyewe wakati muziki ukicheza polepole. Wazia juu ya maskini ujumbe huu uliovunjikavunjika, usimwangalie mjumbe, wazia kile—kile Ujumbe ulicho. Sasa unapojisikia ya kwamba una haja na Mungu, inua tu mkono wako polepole, wakati mmeviinamisha vichwa vyenu, "Bwana, unikumbuke." Sijali unachohitaji. "Unikumbuke, Ee Bwana."

153 Mwaminini Mungu sasa, msitie shaka. Aminini tu. Shikilia haja yako mpaka Mungu anene nawe na kusema, "Nitakupa haja yako."

154 "Bwana, ninasimama nimepofushwa, pia. Ninajionea aibu. Ninasimama, nikikiri kwamba ni Mkristo na kuishi jinsi ninavyoishi, ninajionea aibu. Unirehemu, Bwana. Niponye! Niponye kimwili, niponye kiroho, nifanye Wako. Nilihisi Roho Wako juu yangu. Ndugu Branham alisema ya kwamba Wewe ulikuwa hapa pamoja nasi. Ni—ninaamini sasa, maana nilikuhisi Wewe. Ninajua Wewe upo hapa." Mungu wa Mbinguni atayajibu maombi yako. Amini tu sasa, acha tu Ujumbe uingie ndani yako kabisa. Ombeni tu, iweni na imani. Msitie shaka. Aminini.

155 Sasa, Bwana, nimetoa nafasi hii ya wakati ili wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana wangeweza kutafakari hili. Huu umekuwa ni Ujumbe wa kigeni kwa wengine, hapana shaka, lakini, Bwana, Wewe unajua ni wa kweli. Nikiketi chumbani alasiri ya leo, Wewe—Wewe ulinikumbusha jambo hili, juu ya mtu huyu mashuhuri ambaye wakati mmoja alikuishia Wewe na hali ya mambo aliyoingia ndani yake. Sasa, Baba, kama vile Samsoni alivyokuwa tayari kufa, kufa kwa nafsi yake, kufa pamoja na adui wake, apate kurejesha ushindi wa Mungu na ahadi, tujalie sisi, pamoja na ukanisa wetu wote na tofauti zetu zote, tuyafie mawazo yetu wenyewe, na kulikubali Neno Lako; tuyafie mawazo ambayo tumeambiwa, "siku za miujiza

zimepita," wakati tukijua ya kwamba huyo Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tujalie, Bwana, ya kwamba kusanyiko hili litaona utenda kazi wa mkono wa Mungu mara nyingine tena, na ndipo waje wakatubu, na hapo pawe na mkutano mzuri sana. Pia jalia kutoka kwenye kanisa hili dogo kutokee uamsho ambao utawauwa Wafilisti wote wa mambo ya kilimwengu kote nchini. Pia jalia iwe ni mfano, wakati watu hawa wakiondoka hapa usiku wa leo.

156 Tunaomba ya kwamba Wewe utaingia kama ulivyofanya katika njia ya kwenda Emau. Ulizungumza na watu hao siku nzima. Walikuwa wakizungumza habari Zako. Ulikuwa ukizungumza papo hapo pamoja nao, nao hawakukutambua. Watu wengi hapa, Bwana, huenda kanisani, nao ni waaminifu, na kweli hawajafunzwa vinginevyo. Lakini basi wakati ulipowaingiza chumbani usiku huo na kufunga mlango, Wewe ulifanya jambo fulani jinsi tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa, ndipo wakajua ulikuwa umefufuka kutoka kwa wafu. Waliharakisha wakarudi kwa miguu myepesi na mioyo myepesi, na kuwaambia wanafunzi, kwa mioyo myepesi walisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi njiani?"

157 Jalia hilo litukie mara nyingine, Bwana. Ingia kwenye kusanyiko hili na kufanya mambo uliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, kusudi kusanyiko hili lijue ya kwamba mtumishi Wako asiyestahili hajawadanganya, bali aliwaambia Kweli. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

158 Sasa, tusingeweza kabisa kuitisha mstari wa maombi, kama kadi zipo. Si—sidhani kuna yoyote. Tunazo kadi zilizosambazwa siku chache zilizopita usiku, sidhani walisambaza zozote usiku wa leo. Lakini wanazo kadi hapa. Lakini kama walikuwa nazo, msingeweza kuwa na mstari wa maombi, mnaona, jinsi tulivyovurugika. Sasa, lakini tuta—tutamalizia. Lakini ni watu wangapi humu ndani walio wagonjwa? Hebu tuone mkono wako. Inua mkono wako kama una haja na Mungu. Ama haja ya mtu mwingine aliye mhitaji, inua mkono wako. Ombeni tu.

159 Sasa iweni na kicho. Sasa, hebu tusikose kuupata Ujumbe huu sasa. Sikilizeni. Kama Yesu alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, nawe ungekimbia jukwaani, na kusema, "Bwana Yesu, niponye," unajua kile angekwambia? "Tayari nimefanya hivyo." A*li*jeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tu*li*pona. Gharama imelipwa tayari. Itakubidi kuamini hilo.

160 Unasema, "Lakini laiti ningaliweza kuamini ya kwamba Yeye alikuwa karibu nami, kama nilijua alikuwa hapa! Kama mimi . . . hiyo, hiyo imekuwa miaka elfu mbili iliyopita."

161 Vema, Biblia ilisema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Nasi tungetaka kumwona Yeye. Kama tungeweza kumwona, Yeye angetenda kama alivyotenda.

162 Sasa nitatoa, kwa ajili yenu ndugu wahudumu, Maandiko fulani. Agano Jipya linasema, ya kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu sasa anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli? Yeye alitenda namna gani, ni kwamba wakati alipokuwa duniani Yeye alikuwa ndiye Kuhani Mkuu. Mbona, alikuwa ni zaidi ya hivyo, Yeye alikuwa ni Mungu. Watu wangewezaje—wangewezaje kupata kitu kutoka Kwake? Maskini mwanamke mmoja aliligusa vazi Lake, akaketi chini, ndipo Yesu akageuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Na hao wote wakalikana. Bali ninii Yake. . .Roho wa Mungu aliyekuwa ndani ya Kristo, akimfanya Imanueli, aligeuka mpaka akapata katika kusanyiko maskini mwanamke mmoja, na kumwambia hali yake ilivyokuwa, kasema, "Imani yako imekuokoa." Hiyo ni kweli? Vema, sasa, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, kama ni Kuhani Mkuu yeye yule, Yeye angetenda vile vile.

163 Sasa, ninyi ni wageni kwangu, wengi wenu. Ninamfahamu Ndugu Daulton na hao wengine wanaoketi kwenye kiti hiki cha mbele moja kwa moja hapa, kundi hili papa hapa, maana wametoka huko nyuma Kentucky. Nimewafahamu kwa miaka kadhaa. Na sijakosea, ninaamini huko nyuma kabisa nilimwona Ndugu Gene Goad na Ndugu Leo Mercier, sina hakika. Nina furaha kuwaona ninyi ndugu. Ninamwona Ndugu na Dada Dauch wameketi hapa. Siwataki ninyi watu, kama mna shida yoyote, ngojeni tu, si sasa. Ninataka mtu fulani asiyenijua mimi, nawe unajua sikujui. Ninawatakeni muombe.

164 Ndipo basi kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, wewe liguse vazi Lake, naye Roho Wake Mtakatifu atafanya kazi kupitia sisi. Endapo una mkondo sahihi, Roho wa kuamini kwaye, mkondo ule ule uliopo hapa, atafanya kazi vivyo hivyo. Hana budi kufanya, ni Mungu! Ukiweka uhai wa mtofaa ndani ya mpichi, hautazaa pichi tena, utazaa matofaa. Nawe ukiuweka Uzima wa Kristo ndani ya m—mtu ambaye ni mwanadamu, yeye atazaa tunda la Roho. Atazaa matunda ya ufufuo.

165 Kristo aliuleta Ujumbe huu, na Ujumbe huu—huu kwa Kanisa liuchukue, "Enendeni ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe." Mamilioni hawajausikia bado, mataifa hayajapata kuusikia bado. Kiasi gani? "Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe, ishara hizi zitafuatana na hao waamnio." Umbali gani? "Ulimwenguni kote." Kwa nani? "Kila kiumbe." Hapo ndipo Yeye alipoliagiza kanisa. Sasa nionyeshe katika Maandiko ambapo Yeye alighairi na kuondoa Hilo. Mwanadamu huenda akaingiza wazo lao, bali hilo silo wazo la Mungu. Yeye alisema, "Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe."

63-0120E Mara Nyingine Moja Tu, Bwana
Jesus Name Church
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org